Mbegu Ya Hitilafu

Nimechagua maandiko machache kwa ajili ya usiku wa leo, ama somo fupi, Bwana akipenda, atupe msingi wa somo hilo, kutoka katika Mathayo Mt.13:24 hadi 30. Na halafu pia na—nataka kusoma kutoka 36 hadi 40, katika dakika chache tu. Sasa Mathayo Mt., mlango wa 13, na kuanzia kifungu cha 24 cha mlango wa 13 wa Mathayo Mt. Sikilizeni kwa makini kusomwa kwa Neno. Maneno yangu yatashindwa, lakini Lake halitashindwa.

> *Akawatolea mfano mwingine, akisema, Ufalme wa mbinguni umefanana na mtu aliyepanda mbegu njema katika konde lake;*
>
> *Lakini alipolala, akaja adui yake akapanda magugu katikati ya ngano, akaenda zake.*
>
> *Lakini baadaye majani ya ngano yalipomea, na kuzaa, yakaonekana na magugu.*
>
> *Basi watumwa wa mwenye nyumba wakaenda wakamwambia, Bwana, hukupanda mbegu njema katika konde lako? limepata wapi basi magugu?*
>
> *Akawaambia, Adui ndiye aliyetenda hivi. Watumwa wakamwambia, Basi, wataka twende tukayakusanye?*
>
> *Bali akasema, La; msije mkakusanya magugu, na kuzing'oa ngano pamoja nayo.*
>
> *Viacheni vyote vikue hata wakati wa mavuno; na wakati wa mavuno nitawatuma wavunao, Yakusanyeni kwanza magugu, myafunge matita matita mkayachome; bali ngano ikusanyeni ghalani mwangu.*

2 Je! ulitambua, "Yakusanyeni kwanza magugu, mkayafunge matita matita"? Sasa, nilipokuwa nikisoma haya, kulikuwa na jambo fulani geni lililonijia wakati nilipokuwa nimeketi juu kule kwenye Milima ya Catalina hivi majuzi usiku, nikiomba. Ndipo nikawazia, wapi ningeweza kupata neno ambalo ningeweza kutumia kwa jambo hili nililotaka kunena juu yake usiku wa leo?

3 Ndipo nikashuka nikapata neno *hitilafu*, kwa hiyo nikachukua kamusi na kuangalia maana ya neno *hitilafu*. Nalo linamaanisha ni "kupanda hitilafu," ama—ama, "kuwa kinyume," kama isemavyo Webster, "kupanda hitilafu, kitu cha tofauti," ama, "kuwa kinyume cha jambo ambalo limekuwako tayari." Kwa hiyo nikawazia, somo usiku wa leo, ningeliita: *Mbegu Ya Hitilafu*. Na ninatumaini ya kwamba Bwana atalibariki Neno Lake sasa tunapoliendea.

4 Na pia tunajua Yeye alielezea, katika kifungu cha 36 na—na hadi 43, jinsi mbegu hii ilivyokomaa. Na wakati tukiwepo kwenye jambo hilo, hebu na tusome na hayo pia, kifungu cha 36 sasa hadi cha 43.

> *Na kisha Yesu akawaaga makutano, akaingia nyumbani; wanafunzi wake wakamwendea, wakasema, Tufafanulie mfano wa magugu ya kondeni.*
>
> *Akajibu, akasema, Azipandaye zile mbegu njema ni Mwana wa Adamu;*
>
> *Lile konde ni ulimwengu; zile mbegu njema ni wana wa ufalme; na yale magugu ni wana wa yule mwovu;*
>
> *Yule adui aliyeyapanda ni Ibilisi; mavuno ni mwisho wa dunia; na wale wavunao ni malaika.*
>
> *Basi, kama vile magugu yakusanywavyo na kuchomwa motoni; ndivyo itakavyokuwa katika mwisho wa dunia.*
>
> *Mwana wa Adamu atawatuma malaika zake, nao watakusanya kutoka katika ufalme wake machukizo yote, na hao watendao maasi,*
>
> *Na kuwatupa katika moto, tanuru ya moto: na ndiko kutakuwako kilio, ama kuomboleza na kusaga meno*
>
> *Ndipo wenye haki watakapong'aa kama jua katika ufalme wa Baba yao. Mwenye sikio . . . asikie.*

5 Huyo ni Yesu akiufasiri mfano huo, Mwenyewe, kwa hiyo tunajua basi maana ya fasiri yake. Na sasa tunapoliendea hili, juu ya huku kupanda mbegu na—na kuvuna, sasa Yeye analifasiri. Ndipo basi ninaamini ya kwamba Yesu alikuwa akizungumza juu ya mfano huu katika siku Zake, bali alikuwa akimaanisha uwe ni kwa ajili ya wakati wa mwisho wa ulimwengu, ama, mwisho wa wakati, ambao ni siku *hizi*. Nami ninaamini somo hili dogo usiku wa leo linaambatana sana na majira tunayoishi, kwa sababu Yesu alisema dhahiri kabisa hapa ya kwamba "kule kukusanywa kutakuwa kwenye mwisho wa ulimwengu huu," ya kwamba hapo ndipo mwisho utakapokuwa; kule kukusanywa kwa ngano, na pia kukusanywa kwa magugu na kuyachoma, na kuiingiza ngano katika ule Ufalme. Nami ninaamini hivi ndivyo ilivyokuwa.

6 Na Andiko lingine linaloniongoza kuamini hivi, nililoandika hapa, ni Mathayo 24:24, ambapo limesema ya kwamba, kuzungumza juu ya ki—kiti, mbegu ya hitilafu. Yesu alisema ya kwamba hizo mbegu mbili zingefanana sana hata zingewapoteza walio Wateule kama yamkini. Karibu kufanana kabisa.

7 Mahali pengine katika Maandiko ambapo imeandikwa, ya kwamba mvua humnyea mwenye haki na asiye na haki.

8 Ninakumbuka tukio langu la kwanza nilipopata kuja miongoni mwa Wapentekoste. Nilikuwa huko Mishawaka, Indiana. Nami nilikuwa katika mkutano mkuu, ukumbi karibu kama huu, ambapo wale wa Kaskazini na wa Mashariki walikuwa wamekutana. Kwa sababu ya siku hizo, za ubaguzi, iliwabidi wakutane kule juu. Walikuwa ni madhehebu mawili makuu ya ndugu wa Kipentekoste. Sikuwa nimepata kuwasikia wala kukutana nao hapo awali. Ndiyo mara ya kwanza nilipowahi kusikia kunena kwa lugha. Na mwishoni mwa juma mbili mfululizo, mwa mkutano . . . Mimi nikiwa si mshiriki wao, nilikuwa tu mhudumu kijana tu wa Kibatisti, niliketi huko nyuma kabisa. Na ninakumbuka wakati wa kwanza nilipomsikia mtu ye yote akinena kwa lugha, hata sikujua yote i—ilikuwa na maana gani. Halafu watu hawa wawili, hasa, waliketi mbele, mmoja angenena kwa lugha na huyo mwingine angefasiri yale aliyosema huyo mwingine. Vema, nilianza tu kusoma Biblia yangu kwa bidii sana nilivyoweza, papo hapo, na nikakuta ya kwamba hilo lilikuwa ni la Kimaandiko. Hivyo ndivyo Maandiko, Roho Mtakatifu angefanya hasa.

9 Vema, yapata siku moja baada ya hayo . . . Usiku huo moyo wangu ulikuwa na wasiwasi sana. Nililala kwenye shamba la mahindi. Sikuwa na fedha za kutosha kujipatia ki—ki—kitanda, kwa hiyo nilikuwa tu na pesa za kutosha kwendea nyumbani, ndipo nikanunua donati chache, zimekaa siku chache, ama vinyunya, ndivyo viliitwa hivyo, na kwa ajili ya kiamshakinywa changu. Na nilikuwa nimekaribishwa kula pamoja nao, lakini sikuwa na pesa za kuchangia. Katika siku hizo, hiyo ilikuwa ni katika wakati wa kuzorota kwa uchumi, 1933, kwa hiyo mambo yalikuwa—yalikuwa ni magumu sana. Na kwa hiyo nikawaza, "Vema, nitaninii . . . sitaki kula pamoja nao, lakini ninataka kujua kile walicho nacho. Wao wana kitu nisicho nacho."

10 Kwa hiyo asubuhi hiyo nilikuwa . . . waliniuliza, "Wahudumu wote waje jukwaani na hebu ujitambulishe mtu mwenyewe, wewe ni nani, unatoka wapi."

11 Vema, ni—nilisema tu, "William Branham, mwijilisiti, Jeffersonville," nikaketi. Vema, wakati huo nilikuwa ndimi mhudumu kijana kuliko wote jukwaani. Ndipo kesho yake wakaniita jukwaani nikazungumze. Ndipo baada ya mimi kuzungumza, mbona, tulikuwa na wakati mzuri sana, na ndipo nikaanza kukutana na watu mbalimbali wakinialika kwenye makanisa yao. Basi baada ya wao . . .

12 Baada ya jambo hilo, mbona, nikawaza, "Laiti ningeweza tu kufika mahali walipo watu hawa wawili walio ni nguzo ambao wamenena kwa lugha na kufasiri!" Hilo lilikuwa likinichoma moyoni, nilitaka jambo hilo sana. Vema, kama nilivyowaambia hapo mwanzo, karama ndogo ambayo unavuta. Unajua, karama na miito havina majuto, unavyo maishani mwako mwote,

unaona, unazaliwa navyo, kama ni karama za Mungu. Kwa hiyo sikuzote nilikuwa, tangu nilipokuwa mtoto mchanga, sikuzote lilitukia kwangu, watu wanaonifahamu mimi maishani mwangu mwote, wanajua hilo ni kweli. Vema, kama ningeliwazia... Sikujua ilikuwa ni kitu gani wakati huo, nililiita ono, sikujua hasa ilikuwa ni kitu gani. Lakini niliwazia, "Laiti ningaliweza kuzungumza nao!" Vema, na roho iliyokuwa humo jengoni ilionekana sawasawa kabisa ni Roho ya Mungu kweli.

13 Kwa hiyo ni—nilipata kuzungumza na mmoja wao, na nikamwuliza maswali machache, naye alikuwa ni Mkristo halisi kabisa. Hakukuwa na shaka juu ya jambo hilo, mtu huyo alikuwa ni mwamini halisi. Na mtu yule mwingine, nilipozungumza naye, kama niliwahi kukutana na mnafiki, huyo alikuwa ni mmoja wao. Mtu huyo kweli alikuwa...Mkewe alikuwa mwanamke mwenye nywele nyeupe za rangi ya shaba, naye alikuwa amepata watoto na...watoto wawili kwa mwanamke mwenye nywele nyeusi. Basi nikawaza, "Vema, vipi sasa? Hili hapa, ni—nimechanganyikiwa kabisa. Mimi ni mwamini wa kanuni za kimsingi; lazima liwe ni Neno, la sivyo si sahihi. Na hapa pana Roho yule, mmoja alisikika, kulingana na yote nijuayo mimi, kuwa ni halisi; na yule mwingine alikuwa hana lo lote kabisa; na Roho akiwashukia wote wawili. Sasa, hilo linawezekanaje?" Ningeninii, lilinitatiza.

14 Miaka miwili baadaye, nilikuwa nikiomba katika pango fulani ambapo ningeenda kuomba. Kulikuwa na mavumbi pangoni, na alasiri moja nilitoka, nikaweka Biblia yangu juu ya gogo, na upepo ukaifungua katika Waebrania, mlango wa 6. Ambapo ilisema, ya kwamba katika siku za mwisho, jinsi ingekuwa kama tukianguka kutoka katika Kweli na kujifanya upya tena hata tukatubu, hakukuwako na dhabihu ya dhambi tena, na jinsi ambavyo miiba na michongoma, ambayo mwisho wake ni kukataliwa, ambayo mwisho wake ni kuteketezwa; lakini mvua huinyea nchi, mara nyingi, kuitia maji, kuilima; lakini miiba na michongoma ingekataliwa, bali ngano ingekusanywa. Ndipo nikawazia, "Vema, ilitokea tu kwamba upepo uliifungua hapo." Vema, niliiweka tu Biblia chini tena. Nami nikawazia, "Vema, sasa nitaninii tu..." Na huu hapa upepo unakuja na kuifungua. Jambo hilo lilitendeka mara tatu. Ndipo nikawazia, "Vema, sasa, ajabu hiyo."

15 Halafu nilipokuwa nikiinuka, nikawazia, "Bwana, mbona umenifungulia Biblia hiyo nisome jambo hilo, mimi... nilipofikia mahali hapo, ambapo 'miiba na magugu, ambayo huwa karibu na kukataliwa, ambayo mwisho wake ni kuteketezwa'?" nikawaza, "Mbona, umenifungulia hilo hapo?" Na nilipokuwa nikiangalia nje...

16 Sasa, maono haya ya kweli hutokea bila ya kujichochea kitu. Huyo ni Mungu tu. Unaona? Niliangalia nikaona dunia

iliyokuwa ikivingirika mbele zangu, na nikaona ilikuwa imelimwa. Kulikuwa kuna mtu aliyevaa nguo nyeupe, aliyetoka akaenda akipanda ngano. Na baada ya yeye kwenda kwenye mpindiko wa dunia; akatokea mtu fulani, alionekana wa kuchukiza, naye alikuwa amevaa vazi jeusi, naye alikuwa akitupa mbegu za magugu juu yake kila mahali. Zote ziliota pamoja. Na zilipoota, zote zilishikwa na kiu, kwa maana mvua ilihitajika. Na kila moja ya hizo ilionekana kana kwamba inaomba, huku imeinamisha kichwa chake kidogo, "Bwana, tupe mvua, tupe mvua." Ndipo hayo mawingu makubwa yakatokea, na mvua ikanyeshea zote mbili. Ilipofanya hivyo, maskini ile ngano ikaruka na kuanza kusema, "Bwana asifiwe! Bwana asifiwe!" Na maskini yale magugu yakaruka moja kwa moja upande ule ule, na kusema, "Bwana asifiwe! Bwana asifiwe!"

17 Ndipo hilo ono likafasiriwa. Mvua huwanyea wenye haki na wasio haki. Roho yule yule anaweza kushuka mkutanoni, na kila mtu amfurahie: wanafiki, Wakristo, na wote pamoja. Kweli kabisa. Lakini ni kitu gani? Kwa matunda yao wanajulikana. Unaona? Hivyo ndivyo tu inavyoweza kupata kujulikana.

18 Ndipo unaona jambo hilo sasa, kwa kuwa shayiri mwitu, ama ngano mwitu na nafaka mara nyingi huiga nafaka halisi, ya kienyeji, zinafanana sana hata ingewapoteza walio Wateule. Nafikiri tunaishi katika wakati wenyewe, wakati mambo haya yanapaswa kuhubiriwa na kuzungumzwa.

19 Angalia katika kifungu cha 41, hizo mbili pia zinafanana sana, zinafanana sana katika siku za mwisho hata Yeye hakufanya jambo hilo . . . Yeye asingeweza kutegemea kanisa fulani kuwatenganisha, tuseme, Methodisti ama Baptisti, wala Wapentekoste kuwatenganisha. Alisema, "Yeye atawatuma malaika Zake kuwatenganisha." Malaika yuaja kusababisha utengano, ubaguzi kati ya walio wa kweli na wa uongo. Wala hakuna anayeweza kufanya jambo hilo ila ni Malaika wa Bwana. Yeye ndiye atakayejua yupi ni wa kweli na yupi ni wa uongo. Mungu alisema atawatuma malaika Zake katika nyakati za mwisho. Si Malaika kupitia chini hapa, lakini ni malaika katika wakati wa mwisho, nao wangewakusanya pamoja. Tunajua kwamba huu ni wakati wa mavuno unaokuja sasa. Sasa, *malaika* kwa kweli anafasiriwa "mjumbe." Nasi tunaona ya kwamba kuna malaika saba wa makanisa saba, na sasa . . . La, kupitia zile nyakati za kanisa.

20 Angalia Yeye alisema wapanzi walikuwa ni akina nani, na pia zile mbegu zilikuwa ni akina nani. Mmoja, mpanzi alikuwa ni Yeye, Mwana wa Mungu, aliyetoka akaenda akipanda Mbegu. Ndipo adui akamfuata nyuma Yake, ambaye alikuwa ni Ibilisi, na kupanda mbegu ya hitilafu, nyuma ya ule upandaji wa Mbegu njema. Sasa, enyi marafiki, jambo hilo limetukia katika kila

wakati tangu tuwe na ulimwengu. Kabisa. Kote kote tangu mwanzo, jambo lile lile lilianza.

21 Sasa Yeye alisema, "Mbegu ya Mungu, Neno la Mungu." Yesu alisema, katika mahali fulani, ya kwamba "Neno ni Mbegu." Na kila mbegu itazaa ya aina yake. Na sasa kama Mkristo, wana wa Mungu, wana wa Ufalme wamekuwa ni hiyo Mbegu ya Mungu, basi hawana budi kuwa wao ni Neno la Mungu, Neno la Mungu likidhihirishwa katika wakati wanaoishi, kwa ajili ya Mbegu iliyoahidiwa ya wakati huo. Mungu alitoa Neno Lake hapo mwanzo, na kila wakati umekuwa na Mbegu yake, wakati wake, ahadi zake.

22 Sasa, wakati Nuhu alipojitokeza jukwaani, naye alikuwa ni hiyo Mbegu ya Mungu, Neno la Mungu kwa ajili ya wakati ule.

23 Wakati Musa alipokuja, asingeweza kuja na Ujumbe wa Nuhu, haungefaa kitu, kwa maana yeye alikuwa ni Mbegu ya Mungu katika wakati huo.

24 Ndipo wakati Kristo alipokuja, asingeweza kuja na wakati wa Nuhu ama wa Musa; ilikuwa ni wakati Wake, wa bikira kupata mimba na kumzaa Mwana, Naye angekuwa ni Masihi.

25 Sasa, tumeishi kupitia wakati wa Lutha, wakati wa Wesley (wakati wa Kimethodisti), huko nyuma kote katika nyakati zilizopita, na wakati wa Kipentekoste, na kila wakati umepewa ahadi ya Neno. Na watu wa wakati huo, wanaodhihirisha Neno hilo lililoahidiwa, ndio Mbegu ya wakati huo, kulingana na yale Yesu aliyosema papa hapa, "Hao ndio wana wa Ufalme." Hiyo ni kweli. Dhihirisho la Roho Mtakatifu akifanya kazi kupitia kwa watoto Wake ni Uzao huo wa Ufalme katika wakati huo.

26 Angalia, magugu yalikuwa ndiyo, adui, Shetani, aliyepanda kutoelewana, ama mbe—ama mbegu ya hitilafu, yeye ndiye aliyekuwa na hatia ya kufanya jambo hili la kuchukiza. Shetani alipanda mbegu yake tangu mwanzo, wakati Mungu alipoweka mavuno yake ya awali ya wanadamu juu ya nchi. Adamu, bila shaka, hadi hapo alijua ya kwamba kulikuwa na—na kujua kweli, na kujua mema na mabaya, naye hakuwa amefikia jambo hilo bado.

27 Lakini tunaona, Mungu aliwapa watoto Wake Neno Lake liwe Ngome yao. Ninii yao. . .Hatuna Ngome nyingine zaidi ya Neno la Mungu. Hilo ndilo Ngome yetu. Hakuna mabomu, hakuna makimbilio, hakuna mahali pa kujificha, hakuna cha Arizona wala California, ama po pote pale; kuna Ngome moja tu tuliyo nayo, na hiyo ni Neno. Nalo Neno lilifanyika mwili na kukaa kwetu, ambalo ni Kristo Yesu, Yeye ndiye Ngome yetu pekee. Tukiwa ndani Yake, sisi ni salama.

28 Dhambi hata haihesabiwi kwa mwamini wa kweli. Je! ulijua jambo hilo? Yeye aliyezaliwa na Mungu, hatendi dhambi, hawezi kutenda dhambi. Unaona? Hata haihesabiwi. Mbona, Daudi

alisema, "Heri mtu ambaye Mungu hatamhesabia dhambi." Unapokuwa katika Kristo, huna tamaa ya kufanya dhambi. "Mwabudu, akiisha kusafishwa mara moja, asingejiona tena kuwa ana dhambi," huitamani. Sasa, kwa ulimwengu, huenda ukawa ni mwenye dhambi; bali, kwa Mungu, wewe si mwenye dhambi, kwa kuwa uko katika Kristo. Unawezaje kuwa katika mwenye dhambi wakati uko katika Yeye asiye na dhambi, na Mungu anamwona tu Yeye ambaye wewe uko ndani Yake?

29 Sasa wakati huu wa mavuno. Hapo mwanzo, wakati Mungu alipopanda Mbegu Yake juu ya nchi na kuitoa katika mioyo ya watoto Wake, familia Yake, kutunza Neno hilo, hiyo ilikuwa ndiyo Ngome yao pekee, kutunza hilo Neno! Huyu hapa adui akaja na kuvunja Kizuizi hicho, kwa kupanda mbegu ya hitilafu, kinyume cha Neno la Mungu. Kama hiyo ilikuwa ni hitilafu hapo mwanzo, ingali ni hitilafu! Cho chote kitakachoongeza lo lote kwenye Neno la Mungu, kingali ni mbegu ya hitilafu! Sijali kinatokea wapi, kama kinatokea kwenye madhehebu, kama kinatoka kwa majeshi, kama kinatokea katika nguvu za kisiasa, cho chote ambacho ni kinyume cha Neno la Mungu, ni mbegu ya hitilafu!

30 Mtu anaposimama na kusema yeye ni mhubiri wa Injili, na kusema ya kwamba "siku za miujiza zimepita," hiyo ni mbegu ya hitilafu. Mtu anaposimama na kusema ya kwamba yeye ni mhudumu, mchungaji wa kanisa la mahali fulani, wala haamini ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule katika kila hali (isipokuwa katika mwili wa kawaida), ni yeye yule jana, leo, na hata milele, hiyo ni mbegu ya hitilafu. Anaposema ya kwamba "miujiza na wakati wa mitume ulipita," hiyo ni mbegu ya hitilafu. Wanaposema, "Hakuna kitu kama kuponya Kiungu," hiyo ni mbegu ya hitilafu. Na ulimwengu umejaa hizo. Zinasongamana na kuisonga ngano."

31 Tunaona ya kwamba mpanzi wa kwanza wa mbegu ya hitilafu aliitwa "Ibilisi," nasi tunajua alikuwa hivyo, katika Mwanzo 1. Sasa tunaona ya kwamba, na huku katika—katika Kitabu cha Mathayo, mlango wa 13, Yesu angali anaita hitilafu yo yote dhidi ya Neno Lake kwamba ni "Ibilisi." Na mwaka huu wa 1956, cho chote kinachopanda hitilafu, kinyume cha Neno la Mungu lililoandikwa, ama kinachoweka tafsiri yo yote ya kibinafsi Kwake, ni mbegu ya hitilafu. Mungu hatakubali jambo hilo. Hawezi kukubali. Haliwezi kuchanganyikana. Bila shaka halitachanganyikana. Ni kama mbegu ya haradali; haitachanganyikana na kitu kingine cho chote, huwezi kuizalisha chotara, haina budi kuwa ni kitu halisi. Mbegu ya hitilafu!

32 Sasa tunaona, wakati Mungu alipopanda Mbegu Yake katika Bustani ya Edeni, tunaona ya kwamba ilimzaa Habili. Lakini wakati Shetani alipopanda mbegu yake ya hitilafu, ilimzaa

Kaini. Moja ilizaa mwenye haki; moja ikazaa mwovu. Kwa sababu Hawa alisikiliza neno la hitilafu, kinyume cha Neno la Mungu, ndipo jambo hilo likaanzisha mvingiriko wa mpira wa dhambi papo hapo, na umevingirika tangu wakati huo. Wala hatutaweza kuutoa wote mpaka malaika watakapokuja na kutenganisha kitu hicho, na Mungu awachukue watoto Wake kwenye Ufalme, na magugu yatateketezwa. Angalia mizabibu hiyo miwili.

33 Laiti tungalikuwa na wakati zaidi juu ya somo hili, lakini kugusia tu mambo yaliyo muhimu, tupate kwenda moja kwa moja kwenye kuwaombea wagonjwa katika dakika chache zifuatazo.

34 Angalia, mbegu zao zilikua pamoja hasa tu kama Mungu alivyosema hapa pia katika mlango wa 13, wa somo letu usiku wa leo, la Mathayo, "Acheni vikue pamoja." Sasa, Kaini alienda katika nchi ya Nodi, akajitwalia mke, na kumwoa; naye Habili akauawa, kisha Mungu akamwinua Sethi kupachukua mahli pake. Na vizazi vikaanza kuendelea mbele, kati ya kweli na uongo. Sasa, tunaona wao walikusanyika, kila mmoja wao, wakati baada ya wakati, na ilibidi Mungu kuninii . . . Iliendelea kuharibika sana hata ikambidi Mungu kuiangamiza.

35 Lakini hatimaye walitokea mpaka mbegu hizo mbili, mbegu ya hitilafu na Mbegu ya Mungu, zikatokeza vichwa vyao halisi, na jambo hilo likakamilishwa katika Yuda Iskariote na katika Yesu Kristo. Kwa kuwa, Yeye alikuwa ni Mbegu ya Mungu, alikuwa ndiye mwanzo wa kuumba kwa Mungu. Hakuwa kingine ila ni Mungu. Naye Yuda Iskariote alizaliwa akiwa mwana wa upotevu, alitoka kuzimu, akarudi kuzimu. Yesu Kristo alikuwa ni Mwana wa Mungu, Neno la Mungu lililodhihirishwa. Yuda Iskariote, katika hitilafu yake, alikuwa ni mzao wa Ibilisi, alikuja ulimwenguni, na kwa ajili ya udanganyifu; kama tu vile alivyokuwa hapo mwanzo, Kaini, baba yake wa kwanza.

36 Yuda aliiga tu mambo ya kanisa. Kwa kweli hakuwa mwaminifu, kwa kweli hakuwa na imani (asingalimsaliti Yesu kamwe). Lakini, unaona, yeye alipanda hiyo mbegu ya hitilafu. Alidhani ya kwamba angeweza kufanya urafiki na ulimwengu, mali, na pia afanye urafiki na Yesu, lakini alikuwa amechelewa sana kufanya jambo lo lote juu yake. Wakati ile saa ya mwisho ilipokuja, wakati alipofanya tendo hili ovu, alivuka mstari wa utengano kati ya kwenda mbele na kurudi nyuma. Ilimbidi kuendelea katika njia aliyoiendea, kama mdanganyifu. Alipanda mbegu ya hitilafu, alijaribu kupata kibali cha hayo madhehebu makuu ya siku hiyo, cha Mafarisayo na Masadukayo. Na akafikiri angejipatia sehemu ya fedha, na angependwa na watu. Kama jambo hilo haliwafanyi watu wengi sana kuingia katika hitilafu hiyo, wakijaribu kupata kibali kwa wanadamu!

Hebu na tupate kibali cha Mungu, si cha mwanadamu. Lakini hivyo ndivyo Yuda alivyofanya wakati hitilafu hizi zilipojitokeza kwake.

37 Na tunajua ya kwamba Yesu alikuwa ndiye lile Neno, Yohana Mt. 1, ilisema, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili na akakaa hapa miongoni mwetu." Basi, Neno ni Mbegu, ndipo Mbegu ikafanyika mwili ikakaa kwetu.

38 Kama Yuda alikuwa ni mbegu ya yule adui na ile hitilafu, hiyo pia ilifanyika mwili ikakaa kwetu katika utu wa Yuda Iskariote. Yeye kamwe hakuwa na imani halisi, ya kweli. Alikuwa na kile alichowaza kwamba ni imani. Kuna kitu kama kuwa na imani; na imani ya kujifanya.

39 Na imani halisi ya Mungu itamwamini Mungu, Na Mungu ni Neno, kamwe haitaongezwa cho chote Kwake. Biblia inatwambia kama tukiongeza neno moja, au kutoa Neno moja, sehemu yetu itaondolewa kutoka katika Kitabu cha Uzima, Ufunuo 22:18, mlango wa mwisho wa kumalizia.

40 Katika ule mwanzo kabisa, Kitabu cha kwanza cha Biblia, Mungu aliwaambia wasivunje Neno moja la Hiyo, "kila Neno halina budi kutimizwa," hawana budi kuishi kwa Neno hilo. Yesu, katikati ya Kitabu hicho, akaja na kulinena jambo hilo katika Wakati Wake, na kusema, "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno li—litokalo katika kinywa cha Mungu." Na katika majira ya kufunga ya Ufunuo, tulitabiriwa, ya kwamba "Mtu atakayetoa Neno moja kutoka katika Kitabu hicho, ama kuongeza neno moja Kwake, sehemu yake itaondolewa kutoka katika Kitabu cha Uzima."

41 Kwa hiyo hapawezi kuweko na kitu cho chote kisicho cha hakika, ni Neno tu halisi la Mungu, lisiloghoshiwa! Hao ni wana wa Mungu, binti za Mungu, wasiozaliwa kwa mapenzi ya mwanadamu, wala kwa kupeana mkono, wala aina fulani ya ubatizo; bali wamezaliwa katika Roho wa Mungu, kwa Roho Mtakatifu, na Neno likijidhihirisha lenyewe kupitia kwao. Hiyo ni mbegu halisi ya Mungu!

42 Adui hujiunga na kanisa na kuwa mwaminifu sana katika kanuni ya imani ama cho chote kile. Lakini hiyo si. . .Hiyo ni hitilafu, cho chote kinachoharibu mzao huo halisi wa Kweli ya Neno la Mungu.

43 Basi tunajuaje? Tunasema, "Vema, wao, je! una haki ya kulifasiri Hilo?" La, Bwana! Hakuna mtu aliye na haki ya kufasiri Neno la Mungu. Yeye ndiye anayejifasiria. Yeye huliahidi, kisha analifanya, hiyo ndiyo tafsiri yake. Wakati alipoliahidi, ndipo analitimiza, hiyo ndiyo tafsiri Yake. Cho chote kilicho kinyume cha Neno la Mungu ni hitilafu! Kweli kabisa!

44 Sasa, kama nilivyosema, Yuda hakuwa na imani halisi. Yeye alikuwa na imani ya kujifanya. Alikuwa na i—imani aliyodhani ya kwamba huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu, bali yeye hakujua ya kwamba huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu. Asingeweza kufanya jambo hilo. Na mtu atakayetia shaka kwamba Neno hili la Mungu ni Kweli, yeye ana imani ya kujifanya. Mtumishi halisi wa Mungu atashikilia Neno hilo.

45 Siku chache zilizopita usiku, mhudumu fulani, wa Arizona, wa shule mashuhuri yenye sifa humu jijini, alinijia na kusema, "Na—nataka kukunyosha juu ya jambo fulani" (nikasema . . .) "utakapopata nafasi."

Nikasema, "Hii ndiyo nafasi nzuri sana nijuayo. Njoo huku."

46 Na kwa hiyo akaja, akasema, "Bw. Branham, unajaribu . . . ninaamini wewe ni mwaminifu na ni mkweli, bali unajaribu kuingiza ulimwenguni Fundisho la mitume." Kisha akasema, "Kipindi cha mitume kilikoma wakati wa wale mitume."

47 Nikasema, "Jambo la kwanza ningetaka kukuuliza, ndugu yangu, je! unaamini ya kwamba kila Neno la Mungu limevuviwa?"

Akasema, "Naam, bwana, ninaamini bila shaka."

48 Nikasema, "Basi, ungeweza kunionesha katika Neno ambapo kipindi cha mitume kiliisha? Sasa, nioneshe mahali jambo hilo lilipo, nitaamini pamoja nawe." Kisha nikasema, "Yule mwandishi wa ninii ya mitume, yule aliyekuwa na funguo za Ufalme, kwenye siku ile ya Pentekoste kipindi cha mitume kilipoanzishwa, walisema, 'Waume na ndugu zetu, tufanyeje tupate kuokolewa?' Akasema, 'Tubuni mkabatizwe, kila mmoja wenu katika Jina Lake Yesu Kristo, kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu, kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, na wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.' Sasa, Neno linawezaje kujipinga?"

Mtu huyo akasema, "Nina homa kali sana usiku wa leo."

Nikasema, "Ndivyo ninavyofikiria, pia." Unaona?

49 Sasa hebu niambieni, je! Mungu angali anaita? Kama Mungu angali anaita, basi wakati wa mitume bado ungalipo. Bila shaka! Wengi watakaoitwa na Bwana Mungu wetu, watakaopata kuitwa, watakaoitwa wakati wo wote, wote atakaowaita Yeye, ungali utakuwa ni wakati wa mitume, kwa kuwa Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

50 Sasa, tunaona leo ya kwamba hitilafu hii imepandwa katika kila kipindi. Kama ingaliwezekana kulipata katika dakika kumi ama kumi na tano zijazo, ningefanya hivyo, bali huwezi. Zamani zote katika miaka iliyopita . . . Sisi sote ni nanii, karibu sisi sote tumesoma Biblia. Na sasa kama wakati ule Yesu alipokuja, Naye akakuta ile hitilafu, kinyume. Yeye alikuwa ni

Neno lililodhihirishwa, alikuwa ni tafsiri ya Mungu ya Neno, kwa maana Yeye alisema, "Mnayachunguza Maandiko, kwa kuwa ndani Yake mnafikiri mna Uzima wa Milele, nayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi." Haya basi. Yeye—Yeye alikuwa ndiye tafsiri ya Neno. Na kila mwana na binti wa Mungu aliyezaliwa mara ya pili wa wakati huu ni fasiri ya Neno. Ninyi ni nyaraka zilizoandikwa, zinazosomwa na watu wote. Naam.

51 Angalia, Yeye alisema, "Wananiabudu bure, wakifundisha hitilafu kama Fundisho. Wananiabudu bure, wakifundisha Fundisho la hitilafu, fundisho la mwanadamu, kanuni za imani za mwanadamu, wakifundisha kwamba hizo ni Neno la Mungu, wakati hazina uhusiano wo wote na Neno la Mungu."

52 Angalia, kila wakati ukizaa zao la aina hiyo, kila wakati umefanya jambo hilo, na wetu hauna udhuru. Tuna jambo lile lile, na ni wakati mkuu zaidi wa zao hilo kuliko nyakati nyingine zote zikiwekwa pamoja, kwa kuwa huu ni wakati wa kumalizikia kwa historia ya ulimwengu. Hii ndiyo hitilafu kuu sana iliyopata kuwa juu ya nchi, iko juu ya uso wa nchi leo. Hitilafu katika nyakati nyingine ziliwatoa toka kwa Mungu wa kweli aliye hai, zikawapeleka kwa sanamu. Leo, Yesu alisema katika Mathayo 24:24 ya kwamba ingefanana sana hata ingewapoteza walio Wateule kama yamkini. Nena kuhusu hitilafu! Loo, ni janja sana. Shetani yuko miongoni mwa watu, na ni mwanatheolojia kweli kweli, ni Daktari wa Uungu aliye hodari sana, anaweza kufundisha Neno hilo karibu kikamilifu kabisa. Yesu alisema hivyo. Lakini hebu mwangalie tu, kutakuwako na mahali fulani. Kasema, "Vema, sasa, hilo halikuwa kwa nini hii hii." Loo, naam, ni nini hii, pia, unaona, kwa maana Mungu alisema hivyo.

53 Angalia zilivyofanya. Hitilafu zizo hizo zilileta hasira ya Mungu juu ya siku za Nuhu, wakati Mungu alipompeleka nabii Wake na akahubiri kama moto unaowaka, akawaagiza watu watubu, nayo hitilafu ikazamishwa. Ndipo Shetani alifanya nini? Akafuata moja kwa moja, katika Hamu, na kuanza kuipanda tena. Hiyo ni kweli kabisa.

54 Akaja Musa, yule nabii mkuu, kuwapandisha wana wa Israeli kutoka jangwani. Nini kilitukia? Musa, yule nabii mkuu wa Mungu, akiwaletea Kweli halisi, Kweli iliyodhihirishwa. Alikuwa amekutana na Mungu. Mungu alithibitisha ya kwamba alikuwa amekutana Naye. Na jinsi watu hao huko nyuma, hao makuhani, nao walikuwa na dini zao, ibada zao, kanuni zao na kila kitu, lakini Musa alisimama kama thibitisho la fasiri ya Neno. Usisahau jambo hilo! Musa alikuwa fasiri ya Mungu ya ahadi Yake. Yeye alisema angefanya jambo hilo; alikuwa fasiri ya Mungu.

55 Ni jambo gani lilitukia? Kanisa lilianza tu kutoka Misri, likasimama kwa siku chache, na ni jambo gani lilitukia? Shetani akaja na hitilafu zake katika utu, Kaini wa pili, ambaye

alikuwa ni Balaamu, naye akapanda mbegu ya hitilafu miongoni mwao. Tunajua jambo hilo ni kweli. Ya kwamba Balaamu, mafundisho ya Balaamu, ya kwamba "sisi sote ni ni kitu kimoja, tunamtumikia Mungu yeye yule mnayemtumikia," kimsingi, yeye alikuwa sahihi, kwa maana alitoa sadaka ambayo Mungu alitoa; kondoo dume saba, fahali saba kwenye madhabahu saba, na kuomba kwa Mungu yeye yule kikamilifu kabisa kama vile Musa alivyofanya kule jangwani, namna ile ile kabisa. Bali hawakuwa kitu kimoja! Ikituwekea kivuli cha yale yatakayotukia. Kulikuwako, tena, na Kaini akidhihirishwa katika—katika utu wa Balaamu. Na Mungu alikuwa yuko hapo akidhihirishwa katika utu wa Musa, akifasiri Maneno Yake kupitia kwa mwanadamu, akijitambulisha Mwenywe, ahadi Yake, kupitia kwa mwanadamu. Ndipo hitilafu ikainuka.

56 Ndivyo alivyofanya katika wakati wa Yuda, huyo hapo akaja na hitilafu yake.

57 Pia, kumbukeni, dhambi hii ambayo watu wale waliamini, ya kwamba "sisi sote ni kitu kimoja, tunamwabudu Mungu yule yule, tunapaswa sote kuwa wafuasi wa kanisa moja, tunapaswa kuwa ni watu wa kundi moja," Israeli kamwe hawakusamehewa dhambi hiyo! Yesu alisema, Yeye Mwenyewe, "Wote wamekufa!"

58 Waliangamia, wote ila watatu kati yao, na hao ni wale walioendelea kushikilia na kuiamini ile ahadi. Wakati waoga waliposema, "Hatuwezi kuitwaa hiyo nchi, na ni kazi kubwa sana kwetu," na kadhalika; Kalebu na Yoshua wakawatuliza watu, na kusema, "Sisi tunaweza hata na zaidi kuiteka, kwa maana Mungu alituahidia hiyo! Sijali upingamizi uweje!"

59 Nasi tungali tunaweza kuhubiri uponyaji wa Kiungu, na ubatizo wa Roho Mtakatifu, na bado tuna nguvu za Mungu kututenganisha na mambo ya ulimwengu. Mungu alisema hivyo! Wakati wa mitume haujakoma bado, wala hautakoma, unaendelea mbele.

60 Kwa hiyo, tunamwona mpanzi yule yule wa hitilafu wa zama za kale. Pia kumbukeni, dhambi ile kamwe haikusamehewa. Sasa, ndugu, kama haikusamehewa katu wakati huo, ni vipi sasa wakati mbe—mbegu halisi ya nyakati zote inapokusanyika pamoja?

61 Angalia jambo hili kuu ambalo Balaamu alifanya, lilizidi kuendelea, na hatimaye likaishia katika kuja kwa—kwa Yuda Iskariote, na Yesu. Ilikuwa ni nini? Yuda na Yesu walikuwa tu ni mfano halisi wa Kaini na Habili. Kwa maana, kama vile Yuda alivyokuwa wa kidini, vivyo hivyo na Kaini alikuwa wa kidini. Kaini alijenga madhabahu, akatoa dhabihu, akamwabudu Mungu, alikuwa mwaminifu tu katika hilo kama vile huyo mwingine alivyokuwa. Lakini, unaona, yeye hakuwa na ufunuo wa vile Neno lilivyokuwa. Alidhani Adamu na Hawa walikula matofaa ama tunda fulani. Na Kaini. . .Habili, kwa ufunuo,

alijua hilo lilikuwa ni kosa; damu ndiyo iliyowatoa, ndipo yeye akatoa mwana-kondoo. Ndipo Mungu akashuhudia dhabihu yake ilikuwa ni bora. Ndipo akaona wivu na akajaribu kumwua ndugu yake. Na kama vile alivyomwua ndugu yake juu ya madhabahu ile ile ambayo dhabihu yake ilifia, mwana-kondoo alikufa juu ya madhabahu, vivyo hivyo Yuda Isakariote alimsaliti Yesu Kristo juu ya madhabahu ya Mungu, na akamwua kama vile tu Kaini alivyomwua Habili. Kwa sababu, Kaini alikuwa ni mbegu ya hitilafu.

62 Na vivyo hivyo ndivyo ilivyokuwa Balaamu, yule nabii wa kukodishwa, mtu aliyepaswa kujua vyema zaidi. Na Mungu alimuonya kwa ishara na maajabu, na hata nyumbu akazungumza katika lugha isiyojulikana, na bado aliendelea vile vile. Yeye alizaliwa awe m—mpanzi wa hitilafu.

63 Na kama Yesu alitabiri wakati huu kuishia katika hitilafu iliyo kuu sana iliyopata kuwako, wakati wa kanisa la Laodikia, vuguvugu, lililomtoa kanisani, inawezaje iwe ni kitu kingine ila hiyo hitilafu! Bila shaka, ndivyo ilivyo. Inaishia katika wakati huo.

Na ilikuwa ni Kaini na Habili tena pale Kalvari.

64 Sasa angalia, kama ilivyopata kuwa, mara Yesu alipoondoka, alipopaa Mbinguni, Roho Mtakatifu akatumwa. Huyo alikuwa ndiyo ile Mbegu, Mwenye kulipa Neno Uzima, kama tulivyozungumza jana usiku. Huyo ndiye Mwenye kulihuisha Neno. *Kuhuisha* maana yake ni "kufanya Hai." Roho Mtakatifu aliye halisi hufanya tu Hai Neno ambalo ni Yeye. Hatafanya kanuni ya imani kuwa Hai, Yeye hawezi, kwa maana Yeye si wa kanuni ya imani. Yeye ni Uhai wa Neno la Mungu, kwa kuwa Yeye ni Mungu. Unaona? Naye huuhuisha huo Mwili.

65 Sasa angalia, kama walivyofanya. Halafu, kama vile Biblia ilivyosema, na—na Yohana alinena na watoto wake, na kusema, "Watoto wadogo, mmesikia habari za mpinga-Kristo aliyekuwa aje ulimwenguni," kasema, "ambaye tayari yuko ulimwenguni, na anafanya kazi katika wana wa kuasi." Sasa, hiyo ilikuwa ni kama miaka thelathini baada ya kuja kwa Roho Mtakatifu. Tunaona, wakati Roho Mtakatifu alipokuja, ule Mzao halisi, yule Mpaji-Uhai halisi wa ile Mbegu, ndipo ile hitilafu ikaingia tena. Na angalia, ikaendelea mbele. Ilininii . . .

66 Lile Neno halisi lilikuwa limethibitishwa, hao manabii wa kale walikuwa wamelithibitisha Neno la Mungu kuwa ni Kweli walipokuwa wanaaga dunia. Kama mtu ye yote alipata kusoma lile gombo la Baraza la Nikea, ama la Baraza Lililotangulia Nikea, hizo siku kumi na tano za siasa za umwagikaji wa damu, wakati hilo kundi la Warumi kule chini lilipotaka kuingiza na kuunda madhehebu kutokana na kanisa hilo. Manabii waliingia, wamevikwa ngozi ya kondoo, wakila mboga, nao wakalishindania Neno hilo! Lakini ilifanya nini?

Ilibidi iwe kama Kaini, ilibidi iwe kama Habili, ilibidi mmoja afariki. Bila shaka, ilibidi afe. Na Neno likapoteza ushawishi Wake kati ya watu, nao wote wakalikataa Neno la kweli na kuchukua mafundisho ya sharti ya hitalafu za kanisa Katoliki la mwanzoni. Wakaongeza papa, wakaongeza askofu, wakaongeza *hiki, kile, kinginecho*. Waliondoa maana halisi ya Petro, na ya—ya—ya Maria, na—na hayo mengine yote; na kufanya sanamu, na hawakufanya kitu ila ibada za kipagani kutokana na wanachoita dini ya Kikristo. Ilikuwa ni nini? Mbegu ya hitilafu! Na wakaunda madhehebu, wakaunda madhehebu, kwa mara ya kwanza duniani, kanisa fulani. Ilikuwa ni kitu gani? Hiyo mbegu ya hitilafu ambayo ilianza kupandwa, kitu fulani kikiongezwa, kikiondolewa.

67 Ni nani aliyewahi kusikia, katika Biblia, kutokula nyama Ijumaa? Ni nani aliyewahi kusikia, katika Biblia, juu ya kunyunyizia ko kote badala ya kubatiza, kuzika majini? Ni nani aliyewahi kusikia mambo hayo, "Salamu, Maria" ama cho chote kile? Ni nani aliyewahi kusikia upuuzi huu mwingine mbaya sana wa Waprotestanti hawa, pia? Nyungu haiwezi kusema birika ina grisi. Kweli! Ni ninii tu, aliye na hatia ya jambo dogo sana ana hatia ya mambo yote! Ni nani aliyewahi kusikia Mungu akitenda kazi ndani ya madhehebu? Nioneshe wakati wo wote ambapo moja lilipata kuunda madhehebu na likaendelea kuwa hai. Walikufa mara moja, wala hawakuinuka tena kamwe! Wakati umewadia kwamba jambo fulani litukie, wakati umewadia wa Mungu kutenda kazi. Madhehebu yanaangamiza ushawishi miongoni mwa watu.

68 Jambo lile lile limefanyika leo. Wanaangamiza ushawishi, wanasema, "Loo, kundi hilo la watakatifu wanaojifingirisha, hawana kitu." Na, mbona, ni hitilafu! Kutana na Neno uso kwa uso nawe uone Hilo ni kitu gani, uone kama Mungu hufasiri Neno Lake Mwenyewe. Mungu anaweza kutoka katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto. Amina.

69 Neno lilikuwa limethibitishwa kweli kweli na hao Wakristo wa mwanzoni, jinsi Mungu alivyowaokoa kutokana na kila kitu, na magonjwa, nao walikuwa na manabii, nao walinena kwa lugha, wakafasiri, na wakatoa jumbe ambazo zilitokea kuwa ni kweli kabisa kila wakati. Lakini licha ya Neno hilo lote lililothibitishwa, watu walilikataa Hilo, na kuchagua madhehebu. Huyo ni mama wa madhehebu yote.

70 Zote mbili zimekomaa kabisa sasa. Zilianza kutoa mbegu tena. Ilikufa, bali ikachanua tena katika siku za Luther, kama tunavyojua kutoka kwenye jumbe zilizotangulia hapa katika ile asubuhi ya kiamshakinywa. Ilichanua katika siku za Luther. Sasa wao walifanya nini? Mara baada ya mtu huyo mkuu kufa, waliunda madhehebu.

71 Ilichanua. Na tena katika siku za John Wesley, wakati hao Waanglikana, hata pamoja na usalama wao wote wa milele na kila kitu kilikuwa kimeufunga kufikia mahali ambapo ilikuwa karibu ni ya kuenea mahli pote, basi ni jambo gani lilitukia? Mungu alimwinua mtu fulani jina lake John Wesley, naye akaangamiza kitu hicho chote. Na mara alipokufa, yeye na Asbury na hao wengine, nini kilitukia? Waliunda madhehebu, na sasa una aina mbalimbali za Wamethodisti. Kisha akaja mmoja ama mwingine, Alexander Campbell, John Smith, na kadhalika.

72 Hatimaye, ikatokea Pentekoste, ikitoka kutoka katika aina hizo zote. Nini kilitukia basi? Walipiga mbio vizuri, ni kitu gani kilichowazuia ninyi? Mlirudi moja kwa moja kwenye matope yale yale mlimotoka, mkayarudia matapiko yale yale, mkarudi kwenye hitilafu na kuunda madhehebu, iliwabidi kupatana katika Neno. Na kila wakati Mungu angetuma jambo fulani jipya, msingeweza kulipokea. Hiyo ni kweli! Hitilafu tena! Na, angalieni, kama nilivyosema hivi majuzi, ya kwamba hilo ganda la kwanza dogo lililotoka kwenye shina hili, linatokea likawa majani kisha linakuwa shada, kisha linarudi likawa ubua tena, halafu linatoka. Ganda hilo dogo la ngano linakaribia kufanana sana na punje yenyewe, nasi tulidhani lilikuwa hivyo, lakini unapolifungua, hakuna punje mle ndani hata kidogo. Ni msaidizi tu wa punje kukulia, na linakufa pia, na uhai unatoka moja kwa moja ndani yake na kuingia kwenye punje. Angalia, kwa hiyo wao wanaita makanisa yaliyopanda . . .

73 Tunaona siku hizi kwamba yale makanisa yetu yanayoitwa makanisa, hata Wapentekoste wetu, tulitoka, hatukuweza kuridhika, ilitubidi kufanya makundi yetu wenyewe. Kila kitu kilitokea, ilitubidi kuwa na *hili,* ilitubidi kuwa na *hili*, ilitubidi kuunda kundi lingine. Ndipo jamaa huyu akainuka, akasema, “Yeye yuaja juu ya wingu jeupe.” Mwingine akasema, “A-ha, Yeye yuaja juu ya farasi mweupe.” “Vema, tutafanya vikundi viwili.” Unaona, ni nini? Kupanda hitilafu! Wakati atakapokuja, hata iwe ni nini, Yeye atafasiri Neno Lake Mwenyewe atakapokuja. Hebu tungojee hadi wakati huo. Shika ninii . . . Tukizungumza juu ya jambo hilo, hata hupati Ujumbe wa siku hii. Daima unaelekeza kwenye yale Mungu atakayofanya, ama yale aliyofanya, na kupuuza yale Yeye anafanya. Hivyo ndivyo tunavyopata hitilafu katika jambo hilo.

74 Sasa tunaona ya kwamba leo makanisa yetu, makanisa yetu yote—yote yamepanda upepo, nayo yanavuna tufani. Hatuna mikutano ya maombi, hatuna ibada tulizokuwa nazo. Kuna nini? Tumelegeza mambo kwa kila jambo. Angalia, hata kwa makanisa yetu ya Kipentekoste, yaliyojaa wanawake waliokata nywele zao. Zamani hilo halikuruhusiwa. Nyuso zilizopodolewa, wamepaka rangi kwenye kucha, kila namna ya upuuzi; wanampata mtu hapa nje mwenye . . . Kama akina Rickey na kadhalika; wameoa mara tatu ama nne, na ni

mashemasi; loo, ni hitilafu ya jinsi gani! Ni uchafu! Wanafanyaje jambo hilo? Mungu hataruhusu jambo hilo Kanisani Mwake, inawabidi kwenda kwenye madhehebu wapate kufanya jambo hilo. Mtu fulani ana hofu kusema kitu juu yake, maana watamfukuza atoke katika shirika hilo. Mungu, tupe mtu asiyeunganika na cho chote ila Mungu na Neno Lake, ambaye atasema Ukweli kuhusu jambo hilo. Hilo ndilo tunalotaka hasa. Tumefanya nini? Tumepanda hitilafu. Tumepanda upepo, na sasa tunavuna tufani.

75 Angalia ya kwamba sasa wao wanakusanywa pamoja kwa ajili ya kuteketezwa. Je! Umeng'amua, Yesu alisema, "Kwanza, yakusanye pamoja, yafunge matita matita, kisha uweke matita hayo kwenye lundo moja, Nami nitayateketeza." Kuna tita dogo linaloitwa Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Lutheri, yote yanakusanyika pamoja katika Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Ni kitu gani? "Yakusanye kwanza!" Haleluya! Je! Ulipata kuona, Yeye kwanza anakusanya magugu, anayaondoa kwenye ngano, anayatenganisha, "Yakusanyeni pamoja na mkayateketeze." Yote yatateketezwa kwa hukumu za Mungu, kwa sababu ya kupanda hitilafu kati ya watu, mambo ambayo wao. . .Wenye mfano wa utauwa, na kukana Nguvu zake, wakikana Neno, kushikilia tu baadhi ya taratibu za dini za baadhi ya mfundisho ya sharti ambayo mtu fulani aliingiza ndani yake, akijaribu kuyaweka katika Neno la Mungu. Haitafaa kitu. Ni hitilafu fulani.

76 Ninapaza sauti leo, kama vile ilivyokuwa, yule nabii maarufu wa zamani za kale, Amosi, wakati aliposhuka akaja kwenye ule mji, akasema, "Mimi si nabii, wala mwana wa nabii. Lakini kama simba akinguruma, ni nani asiyeweza kuogopa!" Akasema, "Mungu anaponena, ni nani asiyeweza kutoa unabii." Yeye alibashiri hukumu juu ya kizazi kile, kasema, "Mungu yeye yule mnayedai kumwabudu atawaangamiza ninyi."

77 Wekeni jambo hili, liko kwenye kanda, na mkumbuke. Mungu yeye yule. . .Watu hawa sasa ambao wanakusanya mavuno haya makubwa mno ya—ya Baraza la Makanisa Ulimwenguni, nanyi itawalazimu kuingia humo. Hamwezi kukaa nje yake. Aidha mtaondoka humo mtu mmoja mmoja, la sivyo mtaingia humo. Hakutakuwako na msimamo wa katikati. Itakuwa ni alama ya mnyama. Hakuna mtu angeliweza kununua wala kuuza, ila yeye aliye na ile alama, ama aliye na ile hitilafu. Sasa, tokeni kwake! Tokeni kwake! Ikimbieni! Kaeni mbali nayo! Mungu wanayedai wanamwabudu atawaangamiza. Yule Mungu mkuu wa upendo ambaye hataninii . . .

Wanasema, "Vema, Yesu aliomba ya kwamba sisi sote tunapaswa kuwa mmoja."

78 Halafu Yeye pia alisema, "Mnawezaje kutembea pamoja, watu wawili kutembea pamoja, wasipopatana?" Akasema

"mmoja," kama vile Yeye na Baba walivyo Mmoja. Naye Baba alikuwa ni Neno, Naye alikuwa ni Neno lililodhihirishwa. Alikuwa "Mmoja" pamoja na Baba, kwa maana alikuwa dhihirisho la Neno la Mungu lililoahidiwa. Na ndivyo ilivyo siku hizi, ama siku nyingine yo yote ile. Naam, bwana. Mungu huyo ni Mmoja. Yeye anatutaka tuwe mmoja.

79 Inawezekanaje *hawa* wawe ni mmoja, *huyu* akikana kuzaliwa kibikira, na *huyu* haamini, anakana kuponya Kiungu, na *huyu, yule,* hao wote wakiwa katika mchafuko jinsi hiyo? Wengine wao hata hawamwamini Mungu, hawaamini alikuwa ni Mwana wa Mungu; wanaamini alikuwa ni mwana wa Yusufu, *aliyeitwa* Mwana wa Mungu. Bila shaka. Ndugu pacha wa Walutheri, Wazwingli, wanaamini hivyo, ya kwamba alikuwa ni mtu mzuri tu. Christian Science lilisema Yeye alikuwa ni nabii, mtu wa kawaida tu, kwamba Yeye hakuwa Mungu. Mbona, kama Yeye hakuwa ni Mungu, Yeye alikuwa ni mdanganyifu mkubwa sana ulimwengu uliyewahi kumpata. Yeye alikuwa Mungu la sivyo hakuwa kitu. Alikuwa Mungu! Alikuwa ni Mungu, Mwenyewe, aliyefanyika mwili kati yetu, katika utu wa Mwana wa Mungu. Bila shaka, hivyo ndivyo alivyokuwa.

80 Sasa tunaona hitilafu imeingia. Tunajua ya kwamba iko hapa, hakuna mtu anayeweza kukana jambo hilo. Loo, jamani! Angalia tu. Yeye ataangamiza kundi hilo linalodai linamtumikia Mungu. Wewe tazamia jambo hilo.

81 Mungu alipanda Mbegu Yake. Ninafunga, maana ni wakati wa kuanza mstari wa maombi. Mungu alipanda Mbegu Yake, na Mbegu Yake ni Kristo. Nitahubiri juu ya jambo hilo katika siku chache usiku, mahali ambapo Mungu aliamua kuweka Jina Lake, Bwana akipenda, labda kwenye moja ya viamshakinywa wakati nikiwa na wakati kidogo wa ziada. Angalia, Yeye ndiye njia pekee ya kuepukia. Ndiye Mtawala pekee wa kweli. Ndiye Mungu wa kweli na wa pekee, hakuna mwingine ila Yeye. "Mimi ni Mungu, na Mungu peke yake," Yeye alisema. Yesu alisema, "Hii ndiyo amri: Sikieni, Enyi Israeli, Mimi ndimi Bwana Mungu wako, Mungu mmoja tu. Mimi Ndiye. Kwa nini mnamtafuta mwingine? Mwingine atakuja . . . Nimekuja katika Jina la Baba Yangu, wala hamkunipokea. Lakini mwingine atakuja katika jina lake mwenyewe, naye mtampokea." Nao walifanya hivyo huko Nikea.

"Je! wewe ni Mkristo?"

"Mimi ni Mbatisti."

"Je! wewe ni Mkristo?"

"Mimi ni Mpentekoste."

"Je! wewe ni Mkristo?"

"Mimi ni Mmethodisti," jina jingine.

82 Lakini inapofikia kwenye Jina hilo la "Yesu Kristo," wanaenda mbali sana Nalo wanavyoweza, wao hawataki uhusiano wo wote Nalo, kwa kuwa Yeye ni Neno nalo Neno hujitangaza Lenyewe. Angalia, Mlango pekee wa kutokea! Yeye ni Ua la Uwandani, Biblia ilisema ndivyo alivyokuwa. Kila sifa (katika Biblia) ya Mungu ni ya Yesu Kristo. Yeye alikuwa ni Alfa, Omega, Mwanzo na Mwisho; Yeye Aliyekuwako, ambaye Yuko, na ambaye Atakuyekuja; Shina na Mzao wa Daudi, Shina na pia Mzao wa Daudi; Nyota ya Asubuhi, Ua la Uwandani, Nyinyoro ya Bondeni, Alfa, Omega, Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, yote katika Yesu Kristo! Yeye alikuwa dhihirisho kamili la Yehova Mungu aliyefanyika mwili akakaa kati yetu. Hivyo ndivyo alivyokuwa hasa.

83 Yeye alikuwa Ua la Uwandani. Wao walifanya nini na Ua la Uwandani? Walilikamua, wakaliponda, wapate kupata manukato toka Kwake. Ua zuri halina budi kukamuliwa sana kupata manukato kutoka kwa ua hilo. Na hayo yalikuwa ni Maisha yapendezayo, hakujapata kuwako na maisha yaliyoishiwa kama Yeye, bali ilibidi akamuliwe huko Kalvari.

84 Unaona, wao walichukua u—upako wa Ua la Uwandani na kuuweka juu ya Haruni, ilibidi atiwe mafuta hayo apate kuingia mbele za Bwana katika mahali patakatifu, katika pazia takatifu. Ilibidi atiwe mafuta ya Ua la Uwandani, apate kuingia akanyunyizie kile kiti cha rehema kila mwaka. Na upako huo hauna budi kuwa juu yake, harufu nzuri mbele za Bwana, akibeba damu ya mwana-kondoo mbele zake, baada ya yeye pia kunyunyiziwa na mwana-kondoo. Komamanga na kengele zilizunguka mavazi yake, naye ilibidi atembee kwa hatua fulani, zikiimba "mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu kwa Bwana."

85 Angalia, Yeye ni lile Ua la Uwandani, harufu hiyo nzuri, ule Upako juu ya watu Wake. Huwezi kuja mbele Zake ukiwa na kanuni yo yote ya imani, kitu kingine cho chote, bali umepakwa kwa mafuta ya hilo Ua la Uwandani, lile Neno. Yeye pia ni Yungiyungi la Mabondeni.

86 Sasa, unapataje bangi? Unapata bangi wakati unapochukua yungiyungi na kulikamua, unapata bangi. Madaktari wanaitumia katika maabara zao. Chukua mtu aliye na wasiwasi na mwenye mahangaiko, ama mwanamke, anajisikia kama kwamba ataingia kichaa, anatembea sakafuni na kupiga mayowe, ana wazimu, daktari atachukua bangi yake kidogo ya yungiyungi na kuiingiza ndani ya mkono wake ama ya vena mahali fulani, ama mwanamume, nao watatulia. Imekwisha kwa kitambo kidogo. Lakini mara tu bangi hiyo inapokwisha, hawa hapa wanakuja tena, wakiwa katika hali mbaya kuliko walivyowahi kuwa.

87 Ila nitawaambia, enyi marafiki, hiyo ni mfano tu wa ile Bangi halisi kutoka katika Ua la Mabondeni ninalojua. Yeye

ni Ua la Mabondeni. Alikamuliwa pale Kalvari. Alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa mapigo Yake tumeponywa. Katika huko, huko kukamuliwa kwa maua, Yeye alikuwa ni Ua. Alikuwa Ua kuu sana lililopata kuota, ilikuwa ni hili Ua la Mabondeni, na hili Waridi kuu la Uwandani. Sasa Yeye ananing'inia usiku wa leo, ameangikwa kati ya Mbingu na nchi, ninaamini, alikuwa hivyo wakati huo, hasa, a—apate kuondoa dhambi ya ulimwengu na kurudisha uponyaji kwa ulimwengu. Na Biblia ilisema ya kwamba ni Yeye yule jana, leo, na hata milele.

88 Ewe rafiki, wakati Mungu alipomwambia Musa, kule jangwani, ambaye alikuwa ni m—mfano Wake, amwinue nyoka wa shaba. Na shaba inawakilisha dhambi iliyohukumiwa, nyoka anawakilisha, *nyoka wa shaba* anawakilisha "dhambi iliyohukumiwa tayari." Kama vile, *shaba* ni "hukumu ya Kiungu," kama vile madhabahu ya shaba pale ambapo dhabihu ziliwekwa. Na pia Eliya aliangalia juu na kusema ya kwamba mbingu zilikuwa kama shaba, hukumu ya Kiungu juu ya taifa lisiloamini ambalo lilikuwa limerudi nyuma kutoka kwa Mungu. Shaba inawakilisha hukumu, hukumu ya Kiungu. Na nyoka aliwakilisha dhambi iliyohukumiwa tayari; na Yesu alikuwa ndiye huyo nyoka aliyefanyika dhambi kwa ajili yetu, na akajitwika hukumu ya Mungu. Alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa mapigo yake tunaponywa.

89 Loo, Mungu ana kabati lililojaa Bangi, usiku wa leo, kwa ajili yako. Rafiki Mkristo, wewe u mgonjwa na unaugua. Loo, umechoka, mambo ni magumu sana kwako. Huwezi kuvumilia jambo hilo zaidi sana, uta—utaenda wazimu katika siku hizi tunazoishi.

90 Je! umekwisha kusikia *Life Line* usiku wa leo, kwamba yale waliyosema, ya—ya kwamba Urusi inasema, katika '55, ya kwamba "watachukua mamlaka yote juu ya ulimwengu mzima kabisa"? Kabla jambo hilo halijatokea, Kunyakuliwa hakuna budi kuje. Kwa hiyo kuko karibu jinsi gani, ewe rafiki? Kuko hapa kumekaribia sana.

91 Je! si umtafute Yeye usiku wa leo kwa moyo wako wote? Yeye ni Nyinyoro ya Mabondeni, Naye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Yuko hapa usiku wa leo kujiinua Mwenyewe miongoni mwa watu Wake, kama vile tu Musa alivyoiinua ile—ile ishara ya dhambi, iliyokwisha kuhukumiwa. Wala si dhambi peke yake, pia magonjwa. Kumbukeni, Yesu alisema, "Kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka wa shaba vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuiliwa." Musa aliinua kwa kusudi gani? Kwa ajili ya dhambi, kutokuamini, na kwa ajili ya maradhi. Yesu aliinuliwa juu, pia, kwa ajili ya dhambi, maradhi, na kutokuamini. Yeye alikuwa ni jambo lile lile.

92 Sasa, usiku wa leo, katika siku ambazo tuna hitilafu hii kuu, Yesu Kristo aliahidi katika Luka, ya kwamba katika siku za ninii . . . kabla ya Kuja kwa Bwana, ingekuwa ni kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, na wakati Mwana wa Adamu angejifunua Mwenyewe, kama vile Mwana wa Adamu alivyojifunua Mwenyewe kwa Ibrahimu kule chini; Elohimu, Mungu, aliyefanyika mwili kati ya watu, na akakaa pale pamoja na Ibrahimu na kumwonesha, akamwambia vile Sara alivyokuwa anawazia (huku ameketi nyuma yake) hemani, ambaye hakuwa amewahi kumwona. Akamwambia vile yeye Sara . . . Na akamwita jina lake, "Sara." "Ibrahimu," si ninii yake—si jina lake la Abramu, aliloanza nalo, bali ni Ibrahimu. Si Sarai, S-a-r-a-i; bali S-a-r-a, "Yuko wapi mkeo, Sara?"

Kasema, "Yumo hemani nyuma Yako."

93 Kasema, "Nitakuzuru wakati uu huu mwakani." Naye akacheka. Akasema, "Kwa nini akacheka?"

94 Sasa, Yesu alisema, "Kabla tu ya kukusanywa na kuteketezwa kwa hitilafu hii kubwa, kwamba Mwana wa Adamu atajifunua Mwenyewe katika jinsi ile ile kama alivyojifunua wakati huo." Na hiyo ni . . . Ni kitu gani? Ni kuinuliwa, upya, mbele zenu, kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Unaamini jambo hilo? Hebu na tuinamishe vichwa vyetu basi kwa ajili ya maombi.

95 Mungu mpenzi, tunakupenda. Neno Lako ni mlo m—mkubwa sana kwetu, Bwana. Tunalipenda tu! Tunaishi Kwalo, Bwana. Inaonekana kwamba ujazo wetu hautoshi kamwe. Tunapenda tu kuketi mezani Pako, kwenye Neno Lako, na kufurahia baraka hizo, Bwana, tunapokutanika pamoja namna hii, ndugu na dada ambao wamenunuliwa na Mwana wa Mungu kwa Damu, ambao tumenunuliwa kwa Damu Yako. Nasi tunakuja hapa usiku wa leo, Bwana, tumeziweka wakfu siku hizi za usiku kwa ajili ya kuwaombea wagonjwa. Na kulingana na Maandiko, Wewe ulisema "kwa mapigo hayo sisi tuliponywa." Kwa hiyo si lazima kuomba basi (ni kutubu tu dhambi zetu), kwa maana kwa mapigo Yako tuli-(wakati uliopita)-ponywa. Loo, ni siku ya wokovu ya jinsi gani! Ni—ni ahadi ya jinsi gani ya Imanueli! Kwamba hakika ni Kweli.

96 Wewe ulisema, "Kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona Mimi tena, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa Mimi" (kiwakilishi nomino cha "Mimi") "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Na kwenye ukamilifu wa dahari, ukamilifu huu mkuu wa dahari, Wewe ulisema, kabla tu jambo hilo halijatukia, itakuwa tu kama ilivyokuwa kabla ya moto kushuka Sodoma na kuuteketeza ulimwengu wa Mataifa, ya kwamba kungetokea tena kufunuliwa kwa Mwana wa Adamu kama tu vile ilivyokuwa kule Sodoma. Baba, jalia watu wasilikose.

97 Nami ninaomba, Mungu, kama kitu kidogo ovyoovyo, (kama nilisema vibaya, nisamehe), kuweka gia. Ninawapenda, Bwana. Na—naomba ya kwamba hawatakosa jambo hilo. Jalia huu uwe mmoja wa siku zile za usiku mkuu, Bwana. Jalia kila mgonjwa, anayeteseka, kipofu, ye yote yule aliyeko humu ndani, Bwana, aponywe usiku wa leo. Jalia kila mwenye dhambi aokolewe. Moja kwa moja katika mioyo yao sasa, kama wao hawaamini, na jalia wamkubali Kristo wakati huu. Tujalie, Baba. Yote yamo mikononi Mwako. Tunajikabidhi Kwako, ili tukuone Wewe ukija miongoni mwetu.

98 Nawe ulisema, katika Yohana Mt. 14:12, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Jinsi tunavyojua ya kwamba ulijitambulisha kwa watu, kwa kuwa Wewe ulikuwa ndiye yule Nabii ambaye Musa alisema atainuka. Hawakuwa na manabii kwa mamia ya miaka, hitilafu ilikuwapo kila mahali, bali hata hivyo ilibidi Neno la Mungu kutimizwa; kwa hiyo Neno lilifanyika mwili, na vivyo hivyo hitilafu nayo. Na, Baba, tunaona jambo hilo tena leo, hitilafu ikifanyika lundo moja kubwa; na tunaona Neno likija jinsi ile ile. Tubariki usiku wa leo, Baba. Tunajikabidhi Kwako, pamoja na Neno Lako. Lo lote unalotaka tufanye, lifanye ukitutumia sisi, Bwana. Katika Jina la Yesu. Amina.

99 [Dada fulani ananena katika lugha nyingine. Sehemu tupu kwenye kanda-Mh.] Mwe na kicho sana. Hatujui yale Yeye aliyosema. Huenda anataka kutuambia jambo fulani, kwa hiyo iweni na kicho sana kwa muda kidogo tu. [Sehemu tupu kwenye kanda. Ndugu fulani anatoa tafsiri—Mh.]

100 Amina. Je! mlipata kusoma [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Maandiko ambapo adui alikuwa anakuja, nao wote walikuwa wamekusanyika pamoja, nao . . . adui alikuwa ni jeshi kubwa sana. Ndipo Roho wa Mungu akashuka juu ya mtu fulani, na kumwambia, naye akatabiri, na kusema mahali watakapoenda na kuwavizia, nao wakamwangamiza adui wao. Huyo hapo anakuja tena. Hapo ndipo mahali pa kumwangamizia adui wako, unaona, chukua mkono wa Mungu. Mkono wa Mungu ni Kristo, bila shaka, lile Neno, kwa hiyo chukueni Hilo mioyoni mwenu usiku wa leo tunapoita watu kwenye mstari wa maombi.

101 Ninaamini Billy alitoa kadi za maombi tena leo. B, wenye B, hebu na tuchukue B, themanini na tano. Jana usiku, tulikuwa na kumi na watano jana usiku. Kwa kawaida tunajaribu kuchukua kama kumi na watano kila usiku. Na basi shikeni kadi zenu, tutazishughulikia, sasa. Hebu na tujaribu kama kumi na tano. Themanini na tano. B, kama vile Branham, unajua. B, themanini na tano mpaka mia moja. Nasi . . . Hebu tuone, ni nani aliye na B, themanini na tano, inua mkono wako. Una hakika . . . Loo, huko nyuma, vema, themanini na tano njoo.

102 Sasa, mwanangu. . .Kwa hiyo huenda kukawa na wageni hapa, wasingejua jinsi jambo hili lilivyofanywa. Mwanangu huja huku, ama mtu fulani; kama hataweza kuja, Ndugu Borders, mtu mwingine. Mtu fulani atakuja hapa, na kuzichukua kadi hizi, mia moja ya hizo, kisha akiwa anasimama mbele za watu na kuzichanganya pamoja. Kwa hiyo basi yeye anakupa kadi, hawezi kukwambia utapanda hapa jukwaani, yeye hajui hilo. Na wala mimi sijui. Ninakuja usiku, ninachukua tu kama kumi ama kumi na tano, mahali fulani hapo, katika hizo kadi. Hilo halina uhusiano wo wote na kuponywa kwako. Unaweza kuketi papo hapo. Angalia, jana usiku. Ni wangapi waliokuwa hapa jana usiku, hebu na tuone mkono wako? Jinsi watu walivyoponywa tu kote mkutanoni.

103 Sasa, hiyo ilikuwa ni themanini na tano, themanini na sita, themanini na saba, themanini na nane, themanini na tisa, tisini. Hebu na waje sasa hivi. B, themanini na tano, themanini na sita, themanini na saba, themanini na nane, themanini na tisa, tisini. Huyo angekuwa ni mmoja. . .Hakika, tunahitaji. . .Na kama mtu fulani ananinii. . .Huyu hapa mwingine, naam, hiyo ingelifanya hilo kutimia. Tisini, tisini mpaka mia moja sasa. Tisini, tisini na moja, tisini na mbili, tisini na tatu, tisini na nne, tisini na tano, tisini na sita, tisini na saba, tisini na nane, tisini na tisa, na tisa.

104 Kama huwezi kusogea, kama wewe. . .Ninaona tuna wachache, viti vitatu vya magurudumu hapa sasa, vinne, ninaamini, ninaweza kuona. Kama una kadi ya maombi, kwamba—kwamba namba yako imeitwa, wala huwezi kusogea, inua tu mkono wako, tutakisukuma mpaka hapa.

105 Na kama huna kadi ya maombi, keti tu pale na kuomba, na useme, "Bwana Yesu ja—ja—jalia iwe ni mimi usiku wa leo." Ni wangapi hapa ndani wasio na kadi ya maombi, inua mkono wako. Loo, jamani! Vema, sasa hebu na tuseme tu jambo hili, natumaini halisikiki la kukufuru. Lakini kulikuwa na maskini mwanamke mmoja wakati mmoja ambaye hakuwa na kadi ya maombi, tungesema. Alienda akijipenyeza kwenye umati wa watu, akasema (sasa sikilizeni kwa makini), "Kama ninaweza kugusa vazi la Mtu yule, nitakuwa mzima." Ni wangapi wanaojua hadhithi hiyo? Vema. Naye alifanya nini? Alimgusa, kisha akaenda kule akaketi chini. Ndipo Yesu akageuka, Yeye alijua mahali yule mwanamke alipokuwa. Hiyo ni kweli? Alijua shida yake ilikuwa ni nini. Hiyo ni kweli? Yeye alijua shida yake ilikuwa ni nini, kwa hiyo akamwambia shida yake ilikuwa ni nini. Naye akajisikia mwilini mwake ya kwamba kutokwa kwake na damu kulikuwa kumekoma. Hiyo ni kweli? Kwa sababu gani? Alikuwa amemgusa.

106 Sasa, ni Wakristo wangapi hapa usiku wa leo wanaojua, kulingana na Waebrania, Kitabu cha Waebrania, ya kwamba

Yesu sasa hivi ni Kuhani Mkuu, Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu? Sivyo? Vema, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, huduma ile ile, Kuhani Mkuu, Yeye angetenda vipi basi? Angefanya vile vile kama alivyotenda wakati ule. Mnaamini jambo hilo? Yeye angetenda jinsi ile ile alivyotenda wakati ule, kama unaweza kuamini jambo hilo. Vema. Ni wangapi wanaoamini jambo hilo, inua mkono wako, useme, “Kwa kweli ninaamini jambo hilo”?

107 Vema, kabla hawajafanya mstari wa maombi, hebu na tufanye mstari wa maombi huko mliko. Ninajua Yeye yuko hapa. Ni—ninahisi Uwepo Wake, nami ni—ninajua ya kwamba Yeye yupo hapa. Njoni. Mstari wa maombi uko tayari? Nilikuwa niite huko. Ninyi o—ombeni tu, angalieni huku tu na kuomba, aminini tu.

108 Maskini bibi mmoja ameketi hapa akiningalia moja kwa moja, ameketi kando ya bibi fulani mwenye miwani. Je! huwezi kuona Hiyo ikining’inia juu ya mwanamke huyo? Angalia hapa. Unaona? Yeye ana ugonjwa wa moyo. Je! unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Kama unaamini, inua mkono wako. Hiyo ndiyo iliyokuwa shida yako. Hiyo ni kweli. Sasa kama hiyo ndiyo iliyokuwa shida yako, inua mkono wako watu wapate kuona, inua mkono wako namna hiyo. Sasa, huna huo tena sasa. Imani yako ilikuponya.

109 Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Loo, hiyo hapo hitilafu; lakini Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Je! hii. . . Sasa endeleeni tu kuomba, unaona, si lazima uwe hapa juu, upate kujua.

110 Sasa, huyu ni bibi fulani. Nijuavyo mimi, sijapata kumwona maishani mwangu, yeye ni mwanamke tu anayesimama hapa, naye ana kadi ya maombi, wala hukujua kama ulikuwa uitwe au la. Mtu fulani alikupa tu kadi ya maombi, nawe—nawe namba yako imeitwa, kwa hiyo umekuja tu hapa. Hiyo ni kweli? Nami sina njia ya kujua kwamba wewe unafanya kazi gani, kwamba wewe u nani, unakotoka, unachotaka, sijui lo lote kuhusu hilo. Mimi ni mwanamume fulani tu, wewe ni mwanamke yule. Hiyo ni kweli. Picha ii hii ilitokea wakati mmoja katika Biblia, Yohana Mt., sura ya 4.

111 Sasa mnasema, “Ulifanya nini, Ndugu Branham, wakati huo, muda mfupi uliopita?” Nilitia tu hiyo gia ndogo, unaona. Sijui, unaona. Yeye hana budi kufanya jambo hilo. Sijui. Huyo mwanamke huko nje alifanyaje? Sijapata kumwona mwanamke huyo maishani mwangu. Yeye ni mgeni kabisa kwangu. Ninaamini ilikuwa ni mwanamke. Ni mtu gani aliyeponywa sasa hivi huko kwenye wasikilizaji? Inua . . . Naam. Sisi hatufahamiani. Kama hiyo ni kweli, punga mkono wako namna *hii*. Unaona? Sijapata kumwona mwanamke huyo. Lakini

yeye alikuwa ameketi pale, akiamini. Sasa, yeye aligusa kitu Fulani, sivyo? Haingefaa kitu kunigusa mimi.

112 Lakini sasa je! huwezi kuona ya kwamba Biblia ni Neno la Mungu hasa? Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Sisi tunakuwa maskani ya Roho huyo Mtakatifu ambaye ni Kristo. Unaona? Hiyo ndiyo Mbegu halisi. Basi kama huyo Roho Mtakatifu halisi akiingia kwenye Mbegu halisi ya Neno, si... Hiyo haitachukua sehemu Yake tu (kwa sababu, Ibilisi anatumia Hilo), huna budi kuchukua yote, unaona, kila Neno Lake; maana, Yeye si Mungu nusu, ni Mungu kabisa. Unaona? Na jambo hilo ndilo linalotukia.

113 Sasa, huyu hapa mwanamke, sijapata kumwona. Yesu alikutana na mwanamke kama huyu wakati mmoja, huenda si hali ile ile, sijui. Naye alikuwa ameketi kisimani. A—alitaka ashuke aende Samaria. Nasi tunaona ya kwamba, Samaria ilikuwa chini ya kilima. Na—Naye alikuwa anaenda Yeriko, hasa, naye alizunguka kupitia Samaria, kisha akafika kwenye mji wa Sikari. Basi akaketi chini pale kisimani, akawatuma wanafunzi Wake waende wakanunue chakula.

114 Je! Kuna jamii ngapi za watu ulimwenguni? Watatu: Watu wa Hamu, Shemu, na wa Jafethi. Sote tumetoka kwa Nuhu. Na watu wote waliosalia waliangamizwa wakati huo. Jamii tatu tu za watu, huyo Myahudi, Mmataifa, na Msamaria (ambaye alikuwa ni nusu Myahudi na nusu Mmataifa). Na hizo ndizo jamii pekee zilizopo ulimwenguni, unaona, tatu tu.

115 Kila kitu katika Mungu ni kikamilifu katika utatu. Ni kama tu hizi tatu nilizokuwa nikizungumza juu yake usiku wa leo: hatua tatu za hitilafu, hatua tatu za Neno lililofanyika mwili, kadhalika. Unaona?

116 Sasa, na Yeye—Yeye aliyezungumza na Wayahudi, alimwambia Filipo, wakati alipomleta Nathanaeli, mahali pale alipokuwa, na kusema, "Nilimwona wakati alipokuwa chini ya mtini." Akamwambia... Andrea alikuwa amemleta Petro, Yeye akasema, "Jina lako ni Simoni, nawe utaitwa 'Petro' tangu sasa na kuendelea." Kasema, "Wewe ni Mwana wa Yona." Unaona? Sasa, hao wote walikuwa ni Wayahudi.

117 Bali hapa anamwendea Mmataifa... si Mmataifa, bali Msamaria.

118 Sasa ni wakati wa Mataifa. Yeye hajawahi kufanya jambo hilo hata mara moja kwa Mataifa. Yachunguze Maandiko. Sivyo kamwe. Lakini Yeye aliahidi, katika Luka 22, ya kwamba angefanya jambo hilo kabla tu ya kule Kuja.

119 Lakini Yeye aliketi chini kule, na huyu hapa anakuja nusu Myahudi na nusu Mmataifa, mwanamke. Ndipo akamwambia, "Mama, nipe maji ninywe."

120 Ndipo huyo mwanamke akasema, "Mbona, hupaswi kuomba hayo, kiasi hicho. Sisi ni . . . Kuna utengano hapa. Wewe ni Myahudi, nami—nami ni Msamaria."

121 Akasema, "Lakini kama ungelijua ni Nani unayesema naye, ungeniomba maji unywe." Yeye alikuwa akifanya nini? Akiwasiliana na roho yake. Na mara alipopata kwamba shida yake ilikuwa ni nini, vema, alimwambia aende akamlete mumewe. Akasema hakuwa na ye yote. Yeye akasema, "Hiyo ni kweli, ulishakuwa na watano."

122 Sasa, angalia, wakati Mafarisayo walipomwona akifanya jambo hilo. Kweli, hitilafu hiyo ikiwa moja kwa moja kati ya Neno, wao walisema nini? "Walisema Mtu huyu ni Beelzebuli, mpiga ramli." Unaona?

123 Ndipo Yesu akasema, "Mtu atakayesema jambo hilo juu ya Roho Mtakatifu wakati atakapokuja kufanya jambo lile lile, hatasamehewa kamwe." Hiyo hapo hitilafu yako. Unaona? Lakini Yeye alisema angewasamehe wakati huo, kwa sababu Roho Mtakatifu hakuwa amekuja; ile Dhabihu, Mwana-Kondoo hakuwa amekufa.

124 Lakini basi huyo mwanamke hakufikiri hivyo. Huyo mwanamke alisema, "Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii." Hawajakuwa na nabii kwa mamia ya miaka. Kasema, "Naona kwamba Wewe ni nabii. Sasa, tunajua ya kwamba Masihi, ambaye anaitwa Kristo, wakati atakapokuja, hivyo ndivyo atakavyofanya."

125 Vema, kama hivyo ndivyo alivyofanya, basi yeye yule jana, leo. Hivyo ndivyo alivyojitambulisha wakati huo, si ni jambo lile lile leo? Hana budi kuwa! Sasa, huyu hapa mwanamke na mwanamume wanakutana tena. Yeye siye yule mwanamke, mimi siye Mtu yule. Lakini hata hivyo Roho Mtakatifu yeye yule yuko hapa, naye aliahidi ya kwamba kazi alizozifanya, tungefanya mambo yayo hayo katika siku za kufunuliwa kwa Mwana wa Adamu.

126 Sasa, mimi nikiwa sikujui (nawe unajua hiyo ni kweli), sisi hatufahamiani kabisa, nawe unasimama hapa. Kuna baadhi . . . labda una tatizo, labda kuna, sijui mimi. Lakini kama Bwana Yesu atanifunulia, kwa Roho Wake Mtakatifu, shida yako ni nini, je! utaamini basi ya kwamba Huyo ni Mwana wa Mungu, wala si mwanadamu? Hili ni ganda tu, maskani hii ambayo—ambayo Mungu anatumia, ye yote ambaye Yeye amemchagua. Yeye—Yeye anafanya jambo hilo kwa neema yake kuu na uteuzi. Kwa hiyo, lakini wewe amini. Sivyo? [Mwanamke huyo anasema, "Amina"—Mh.]

127 Ni wangapi katika wasikilizaji wataamini jambo hilo? Sisi hapa wawili tumesimama papa hapa mbele ya ile Nuru, ambao hatujakutana katika maisha haya, sina wazo lo lote kwamba mwanamke huyo ni nani, kwamba yeye ni nini, anatoka wapi,

anataka nini. Sijapata kumwona maishani mwangu, si zaidi ya nilivyopata kumwona mwanamke yule *pale* chini maishani mwangu. Lakini, unaona, hivi ndivyo ninavyojaribu kuwafanya mfanye: ondoleeni mbali hiyo hitalafu, na mwamini Neno wakati Neno linapofanyika mwili papa hapa kati yetu. Neno linakuwa hai katika miili yetu wenyewe, jambo hilo linaonesha Uwepo wa Mungu.

128 Sasa na amjalie haja yake. Yeye anataka jambo linalostahili. Hana mtoto, anataka mtoto. Ana umri wa miaka arobaini hivi. Hilo bila shaka si lisilowezekana.

129 Wapo wameketi moja kwa moja huko nje sasa, wanawake waliokuwa tasa maishani mwao mwote, nao wakaja jukwaani namna hii, na Bwana akawapa watoto. Baadhi yenu inueni mikono yenu huko ambao mnajua. Unaona? Unaona? Niliinua kisichana kidogo kipenzi hivi majuzi, Jumapili, baada ya mimi kuondoka hapa, Jumapili alasiri; ambaye mama yake alikuwa ni tasa, Bwana akanena. Na maskini msichana huyo mdogo, anayependeza mno, je! yuko hapa? Yuko wapi? Naam. Huyu hapa, papa hapa, ameketi papa hapa chini. Mamaye ameketi pale. Huyu hapa huyo msichana mdogo, mwenyewe. Mnamwona? Yeye alikuwa ni Neno lililonenwa kutoka kwa Mungu.

130 Sasa je!, utamwamini Yeye kwa moyo wako wote? Je! unaamini ya kwamba baraka hizo ulizo nazo, unazosikia ndani yako sasa, zimekuwa ni Mungu akijibu? Kama Mungu angeniambia jina lako ni nani, ili upate kumpa jina mtoto huyo, je! ungeamini? Basi, Bibi Thompson, unaweza kwenda nyumbani ukampate mtoto wako, kama utaamini kwa moyo wako wote.

131 Je! unaamini kwa moyo wako wote? Uwe na imani tu, usitie shaka, mwamini Mungu tu. Mungu ni Mungu.

132 U hali gani, bwana? Nadhani sisi hatufahamiani, pia. Wakati pekee niliopata kukuona maishani mwangu, nijuavyo mimi, ni wakati ulipokuwa unakuja pale. Nami nilidhani ulikuwa ni mjomba wa Ndugu Shakarian, ama ye yote yule . . . Mashagian, Ndugu Mashagian, yule mwimbaji, ulipokuja hapa. Ndipo nikaona ulikuwa ukienda kwenye mstari wa maombi. Sasa, nikiwa mgeni kwako, na, ama kwako, nami nikiwa mgeni, vyo vyote vile. Sasa, kama Bwana Yesu ataniambia jambo fulani ambalo umeninii—jinsi ulivyo, kile unachohitaji, hebu na tuseme hivyo tu; akwambie nini, aniambie unachotaka. Sasa, Yeye ameshakupa hicho tayari. Jambo pekee ni imani tu ya kutosha kuamini jambo hilo.

133 Sasa, ni wangapi wanafahamu jambo hilo? Imani ya kutosha tu kuamini ya kwamba unapata unachoomba! Unaona?

134 Sasa, sasa, kama uko hapa unataka jambo fulani, Naye anaweza kuniambia haja yako ni nini, halafu ujue mimi sijui haja yako, basi haina budi kiwe ni kitu Fulani hapa kinachofanya jambo hilo. Sasa, kulingana na Neno, Yeye aliahidi

kufanya jambo hilo. Alijua mawazo ndani ya mioyo yao. Hiyo ni kweli? Vema.

135 Una shauku kubwa ya kuponywa. Jambo moja, unasumbuliwa na hali ya wasiwasi, una wasiwasi mwingi kweli. Hiyo ni kweli. Jambo lingine, una shida ya mgongo, na mgongo huo umekuwa na hali mbaya sana kwa muda fulani, hata umefanyiwa upasuaji wake. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli. Unaona. Hiyo ni kweli. Na hili hapa jambo lingine, haja yako kubwa, ni, unataka kupokea ubatizo wa Roho. Hiyo ni kweli kabisa. Njoo hapa.

136 Mungu mpenzi, katika Jina la Yesu Kristo, mtu huyu na ajazwe na Roho Mtakatifu, kabla hajaondoka mahali hapa, katika Jina la Yesu. Amina.

Sasa mpokee, ndugu yangu. Uwe tu na imani, usitie shaka.

137 U hali gani? Ninadhani, kadiri nijuavyo mimi, ya kwamba sisi hatufahamiani mmoja kwa mwingine. Kama hiyo ni kweli, mbona, ili kwamba watu wapate kujua, inua tu mkono wako ili waone kwamba sisi hatufahamiani. Sijapata kumwona maishani mwangu, kwa kumjua. Nami nadhani hajapata kuniona, isipokuwa iwe ni huko kwa wasikilizaji. Kwa maana Baba wa Mbinguni anajua, na hili hapa Neno Lake limewekwa hapa, ya kwamba sijapata kumwona mwanamke huyo, kumjua, maishani mwangu. Kwa hiyo, nisingejua kilichokuleta hapa, sina fununu kwamba wewe ni nani, nini, wala cho chote kukuhusu wewe. Nisingeweza kukwambia hata jambo moja.

138 Jambo ni kwamba, ni kipawa tu. Kama ninaweza . . . Kama ulivyonisikia nikielezea jambo hilo muda mfupi uliopita. Ninasogea juu tu, ninasikia yale Yeye anayasema; yale ninayoona, ninaweza kuyasema. Yale ambayo hasemi, siwezi kuyasema. Ningalisema hayo mimi mwenyewe, na ingekuwa ni makosa. Unaona? Ingekuwa ni makosa. Lakini kama Yeye akisema jambo hilo, ni kweli kabisa. Haiwezi kamwe, kamwe halijapata kuwa makosa. Kamwe halitakuwa makosa mradi tu inadumu kuwa ni Mungu. Unaona? Unaona, kwa maana Mungu hawezi kukosea.

139 Lakini kama Mungu anaweza kuniambia unachotaka, shauku yako ni nini, ama—ama kilichokuleta hapa, jambo fulani ambalo umefanya, ama cho chote kile, kitu kama hicho, ama kwamba wewe ni nani, unatoka wapi, ama cho chote anachotaka kuniambia, ungeweza kuamini? Asante.

140 Jambo moja, una shida ya miguu yako. Miguu yako inakusumbua. [Mwanamke huyo anasema, "Naam"—Mh.] Hiyo ni kweli. Inua ninii wako . . . Una shida ya kike, ugonjwa wa kike. ["Naam."] Nawe unahitaji kubwa moyoni mwako, kwa maana hivi karibuni umepoteza mtu fulani ama kitu fulani. Ni mvulana, na mvulana wako ameondoka nyumbani, akatoroka, nawe unataka niombe ya kwamba atarudi. ["Naam."]

141 Mungu Mbinguni, mrudishie mtoto wake. Jalia Roho Mtakatifu amzuie mvulana huyo barabarani usiku wa leo, amrudishe kwa mama yake. Katika Jina la Yesu. Amina.

142 Yeye anayejua atamrudisha kwako. Usihofu. Amini sasa, usitie shaka. Uwe tu na imani, moyo wako wote. Wewe amini, Na Mungu atakujalia hayo mengine.

143 Sasa, pambanuzi hizo tatu au nne, cho chote kile, unaona, ni—nilienda tu mpaka nikawa sioni. Siwezi kueleza jambo hilo, hakuna njia ya kulielezea. Unasema, "Unataka kusema, kiasi hicho tu kilikufanya uone hali mbaya zaidi ya kuhubiri pale kwa muda wa dakika arobaini na tano ama zaidi, unafikiri?" Naam, bwana. Kama ingalikuwa ni saa tatu, haingekuwa kiasi hicho.

144 Mwanamke mmoja aligusa vazi la Bwana wetu Yesu. Na hao watu hawanigusi mimi. Mbona, mwanamke huyu hapa, hebu angalieni tu hapa, angeweza . . . [Ndugu Branham anamwambia huyo mwanamke, "Weka mikono yako juu yangu, unaona."—Mh.] Yeye alinigusa tu kila mahali, halingefanya kitu cho chote, mimi ni mwanadamu tu. Bali hana budi kumgusa Yeye. Nami, kwa karama, ninii tu—ninii tu . . . inaondoka tu, mimi mwenyewe mzima huondoka, nami ninasema tu ninachoona. Unaona? Na ni hivyo tu. Unaona, kunigusa mimi hakumaanishi kitu, bali mwanamke huyo anamgusa Yesu kupitia mimi. Hivyo ndivyo yule mwanamke alivyomgusa Mungu kupitia kwa Yesu, wakati Yeye hakujua shida yake ilikuwa ni nini. Aligusa tu vazi Lake, akaenda na kuketi chini. Ndipo akasema—ndipo akasema, "Ni nani aliyenigusa?"

145 Ndipo mitume wakasema, "Mbona, kila mtu anakugusa. Kwa nini unasema hivyo?"

Akasema, "Lakini ninaona kwamba nguvu zimenitoka?"

146 Sasa, mnajua uwezo ni kitu gani? Nguvu. Yeye aliishiwa nguvu kwa kuguswa na mwanamke mmoja, Naye alikuwa Mwana wa Mungu. Je! na mimi je! mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema Yake? Unajua ni kwa sababu gani hiyo ni zaidi? Ni kwa sababu Yeye alisema, "Mambo haya nifanyayo Mimi, ninyi nanyi mtayafanya. Mengi kuliko haya mtayafanya, kwa maana Mimi naenda kwa Baba Yangu." "Kubwa kuliko," Hilo lilisema pale, lakini tafsiri sahihi ya Kiyunani ni, "Nyingi kuliko hizi mtazifanya."

147 Sasa, huyo bibi simjui. Sijajua kitu juu yake. Yeye ni mgeni kabisa kwangu kama vile watu hao wengine walivyokuwa. Sisi ni wageni mmoja kwa mwingine. Ili kwamba tu watu wapate kujua jambo hilo, unaweza kuinua mkono wako, useme "sisi hatufahamiani." Sasa, Mwana wa Mungu, kama Yeye wakati mmoja alikutana na mwanamke katika mandhari madogo kama haya, karibu na kisima, Naye akasema naye kwa muda kidogo tu, ndipo akajua shida yake ilikuwa iko wapi, Naye akamwambia shida yake ilikuwa ni nini. Na kwa hiyo akajua kwa jambo

hilo, ya kwamba huyo alikuwa ni Masihi. Sasa kwa kuwa—kwa kuwa nimeninii . . . Wewe umenigusa, mimi nimekugusa, na hakuna kitu kilichotukia. Lakini kama imani yangu (kwa karama fulani) na imani yako (kwa kuiamini) naweza kumgusa Yeye, Naye anaweza kunena kupitia kwetu kuninii . . . kwako kupitia kwangu, ndipo unajua ya kwamba Yeye yuko hapa kama alivyokuwa kwenye kile—kile kisima Sikari. Unaona? Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Unaamini jambo hilo?

148 Una shida nyingi sana, mateso mengi sana, matatizo! Moja ya mambo muhimu unayotaka kuombewa ni yabisi kavu. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli? Unakakamaa kwa yabisi kavu. Unapoona ukiinua mkono wako . . .

149 Nawe kwa namna fulani ulitembea pole pole, sana sana ninavyokumbuka mimi. Labda ngoja kidogo, labda jambo lingine linaweza kusemwa litakalochukua ninii . . . Ama unajua, unasikia mambo; watu, unajua, kama kwamba ni pumzi ikija dhidi Yake. Wao wanasema, "Mbona, yeye alikisia hilo," ama, unajua, mambo ya namna hiyo.

150 Lakini, unaonekana kuwa u mtu mzuri, hebu nizungumzie tu kwa muda kidogo. Hebu na tusimame hapa kidogo tu, kwa maana ninafikiri kuna jambo lingine moyoni mwako unalotaka kutoka kwa Mungu. Sasa, nisingeweza kujibu sala yako, lakini Yeye anaweza kunifunu- . . . Kwa sababu, kama unaamini, limejibiwa tayari. Lakini kama unataka tu kuamini; kukufanya uamini. Sasa, ninakwambia, ni kuhusu mpendwa mmoja ambaye hayupo hapa, na huyo ni kaka yako, na huyo kaka hata hayuko katika nchi hii. Yeye yuko katika kitu kama nchi yenye maji maji, maziwa mengi. Ningesema ni kitu kama Michigan ama ninii fulani . . . Naam, mahali penyewe ni Michigan. Naye anaugua ugonjwa mbaya sana wa kufisha, na huo ni shida ya figo isiyotibika ambayo inamsumbua. Hiyo ni kweli, sivyo? Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Sasa, leso uliyo nayo mkononi mwako, ambayo ulimwinulia Mungu, itume hiyo kwa kaka yako na umwambie asitilie shaka, bali aamini, na hiyo itaninii, atapona, sasa ni kama utaamini jambo hilo.

151 Unaamini kwa moyo wako wote? Unaona, basi, kama unaamini, kuna jambo moja tu la kufanya, hilo ni, kubali jambo hilo kabisa. Hiyo ni kweli?

152 Sasa mnasema, "Yeye anaangalia jambo hilo, hao watu. Hivyo ndivyo anavyofanya, anawaangalia." Unaona jambo hilo sana!

153 Bali ili kwamba msipate kujua jambo hili . . . bibi huyu hapa, njoo huku, bibi, hapa, mgonjwa, hata uwe ni nani. Mimi simwangalii yeye. Je! unaamini ya kwamba Mungu anaweza kunifunulia mimi kwamba shida yako ni nini? Inua mikono yako, kama unaamini, bibi huyu hapa, bibi huyu hapa, aliye mgonjwa. Naam. Naam. Vema, basi kama utaamini jambo hilo

kwa moyo wako wote, shida hiyo ya yabisi kavu haitakusumbua tena. Vema, nenda nyumbani na uamini jambo hilo . . . ? . . .

154 Sikumwangalia, sivyo? Unaona, Yeye . . . Angalia upande *huu*, ono liko pale hata iweje. Amina! Hivi hamwezi kuliona? Kamilifu tu kama vile Mungu anavyoweza kuwa mkamilifu!

155 Unaamini, pia? Pumu inaweza kukuacha, pia, sivyo? Unaamini itakuacha? Vema, nenda ukamwambie Bwana Yesu Kristo ya kwamba u—unamwamini.

156 Siku moja itakubidi kubeba fimbo ndo—ndogo ukienda huku na huko kama hiyo yabisi kavu ikikulemaza, lakini haitakulemaza. Huaninii, huamini itakulemaza, sivyo? Unaamini utapona? Nenda zako nyumbani, na Yesu Kristo anakuponya.

157 Ugojwa wa moyo huua watu, bali si lazima ukuue. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya na huo, na kukufanya mzima? Nenda ukiamini kwa moyo wako wote, useme, "Kweli ninaamini jambo hilo."

158 Je! unazungumza Kiingereza? Unafahamu Kiingereza? [Ndugu Branham anasema, "Mtu fulani na aje." Mkalimani fulani anakuja—Mh.] Naam, vema. Je! utamwambia ninayomwambia? Mwambie kama ataamini, ugonjwa wa tumbo utamwacha. A—ataamini? Shida yako ya mgongo itakuacha, pia, kwa hiyo sasa unaweza kwenda zako nyumbani na uwe mzima.

U hali gani? Unaamini? [Anasema, "Naam, bwana."—Mh.]

159 Mtu yule anayeketi pale akiwa na shida ya mgongo, akiniangalia niliposema hivyo. Yeye anaweza kuponywa, pia, kama ukiamini jambo hilo, bwana. Vema, bwana.

160 Bibi anayeketi karibu nawe kabisa pale, una shida ya shingo, sivyo, bibi? Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Unataka kuweka mikono yako juu ya mavulana huyo mdogo kwa ajili ya magoti yake, naye atapata afya, pia. Unaamini jambo hilo? Ulikuwa na ugonjwa wa kike, ugonjwa wa akina mama, hunao sasa. Imani yako ilikuponya na kukufanya mzima.

161 Unaamini Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele? Basi hebu na tuwekeane mikono yetu mmoja juu ya mwingine na tuombe sala hili ya imani, kila mmoja wetu, tuombe maombi ya imani.

162 Mungu mpenzi, wakati tumefunikwa sana katika Uwepo Wako wa Kiungu, kukuona Wewe ukitembea katika wasikilizaji, ukiwaponya wagonjwa kila mahali. Wewe ni Mungu. Ninaomba ya kwamba utawaponya wasikilizaji hawa wote. Jalia Pumzi ya Mungu ishuke upya ndani ya mioyo yao, na jalia wao wajue ya kwamba wakati unakwisha. Tutakaa muda kidogo tu hapa, ndipo tutaenda kuwa pamoja Naye Yeye tunayempenda. Na sasa jalia Uwepo Wake ulete uponyaji kwa kila mtu.

163 Tunamlaani Shetani, Tunalaani matendo yake yote. Katika Jina la Yesu Kristo, Shetani, watoke watu hawa.

164 Wote watakaomwamini Yeye sasa, na mnakubali uponyaji wenu, simameni kwa miguu yenu, semeni, "Sasa ninasimama kukubali uponyaji wangu. Ninaamini jambo hilo." Haidhuru hali yako ikoje, kama unaamini jambo hilo kweli kweli, simama kwa miguu yako. Sasa inua mikono yako, na useme, "Asante, Bwana Yesu, kwa kuniponya." Mungu awe pamoja nanyi.

Mbegu Ya Hitilafu SWA65-0118
(The Seed Of Discrepancy)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatatu jioni, 18 Januari, 1965, katika Westward Ho Hotel kule Phoenix, Arizona, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 2003 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2003 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org